Ujumbe Wa Neema

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Habari za asubuhi, marafiki. Bila shaka ni baraka kuwa hapa tena asubuhi ya leo katika ibada ya Bwana. Na tunasikitika sana kwamba hatuna nafasi yoyote ya kuwaweka watu katika kanisa hili dogo. Halienei watu wengi. Lakini tuna furaha sana kwamba mpo hapa na mko radhi kujitolea, ku—kuwa na subira kutungojea. Nasi tutafanya vizuri tuwezavyo kuwaletea Neno la Bwana vizuri sana tujuavyo kulileta. Na sasa ninaninii tu . . .

2 Maskini mwanamke huyu anayeingia, naye alikuwa na mtoto wa kuwekwa wakfu asubuhi ya leo, halafu akaona ya kwamba kwa namna fulani walikuwa wakichelewa, naye akasema atangojea tu. Sijapata kumwona mwanamke huyo hapo kabla, bali ninaomba ya kwamba Mungu atambariki na kumpa baraka Zake zilizo na utajiri mwingi kupita zote moyoni mwake, kwa sababu ya kuwa na subira kungojea.

3 Sasa, yanakuja majira ya mwaka ambapo itakuwa baridi zaidi wala haitakuwa na joto sana wakati tumesongamana sana kanisani. Nasi tunatumaini ya kwamba Mungu atawabariki sana ninyi nyote.

4 Sasa ningetaka kusema mambo machache tu hapa kabla tu sijahubiri. Nilikuwa nimetangaza ya kwamba nitazungumza asubuhi ya leo, Bwana akipenda, juu ya somo la *Zile Pepo Katika Upepo Wa Kisulisuli*. Lakini Yeye alinibadilishia hilo tu. Huwa sijui kile nitakachosema mpaka labda dakika chache tu kabla ya kuja mkutanoni. Nami nililijaribu somo hili kwa mara ya pili, na nikashindwa kupata jibu kutoka kwa Mungu. Sijui ni kwa nini. Daima mimi hupenda, kama vile ninyi nyote wahudumu hapa mjuavyo, ya kwamba huna budi kumngojea Bwana kwa yale utakayosema.

5 Jana usiku kwenye simu ya binafsi, nilipata si—simu iliyokuja umbali huo wote kutoka mahali fulani huko chini Arkansas, watu fulani walitaka kuhamia huku juma hili lijalo, wakasema walisikia tutaanza mkutano juu ya *Mihuri Saba*. Ndiyo kwanza nimalize *Nyakati Saba Za Kanisa*, kwa wageni. Naye mumewe anakuja Jumatatu kutafuta kazi huko Louisville, apate kufanya kazi wakati wakiishi karibu vya kutosha kuisikiliza hiyo *Mihuri Saba*. Nikasema, "Hiyo ingechukua kama miezi mitatu, mama. Hatuna mahali popote hapa pa kuutangazia mkutano huo, na kadhalika, hakuna kitu cha kukidhi mahitaji yake hapa mjini, hakuna mahali pa watu kuketi."

6 Ningetaka wakati mwingine, labda, kama Mungu akipenda, kufanya hayo huko nje kwenye uamsho mahali fulani, tupange

mkutano wa karibu miezi mitatu na tuanze kupitia moja kwa moja kwenye hiyo mihuri namna hiyo, huko nje katika uamsho. Ndipo watu wangeweza kukaa huko hata mwisho wake.

7 Humu ndani, inaanzia kwenye mlango wa 6 wa Ufunuo, mpaka wa 19. Hivyo unapata ile mihuri saba, yale mapigo saba, zile ole tatu, yule mwanamke aketiye juu ya mnyama mwekundu sana, na wale mia moja na arobaini na nne elfu. Loo, kuna mengi sana yake yanayoenda kuyafunganisha hayo kabla ule Mhuri wa Saba kutolewa, pigo la saba linaanguka, baragumu ya saba inalia. Na kuna mengi sana ya hayo ambayo yote yanafunga hilo pamoja, na kila moja la hayo lenyewe ni ujumbe mkuu wa siku nzima.

8 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi kwa maombi mafupi. Kabla hatujaomba, je! kungekuwako na wengine hapa ndani wangetaka kukumbukwa katika maombi haya, na mngeonyesha kwa kuinua mikono yenu. Na moyoni mwako, umwazie Mungu kile tu unachohitaji sasa. Nami ninaomba ya kwamba Yeye atakupa.

9 Mungu mwenyezi na Mwenye Rehema, ambaye ni Mungu anayejibu maombi, Baba anayejua haja zote za watoto Wake. Wewe ulitujua kabla hatujazaliwa, Nawe umezihesabu hatua za miguu yetu, nywele zenyewe za vichwa vyetu zimehesabiwa, nayo maneno yetu yote yamepimwa kwenye mizani Yako. Kwa hiyo, Bwana Mungu, tujalie asubuhi ya leo tuyatilie maanani mambo haya, jukumu hili takatifu tulilo nalo mbele Zako.

10 Mingi ya mikono hiyo iliyoinuliwa asubuhi ya leo, hapa katika kusanyiko hili dogo, labda ilikuwa ni kwa ajili ya maombi ya miili yao migonjwa, mpendwa aliyepotea. Wewe unaijua mioyo yao na yote yaliyo ndani yao. Kwa kuwa, wakati Wewe uliposimama hapa duniani, katika umbo la mwanadamu aliyeitwa Yesu, Bwana wetu, ulijua siri yenyewe ya moyo. Kila kitu ambacho watu wangekiwazia mioyoni mwao, Wewe ungewaambia moja kwa moja kile walichokuwa wakiwazia, "Mbona mnafikiri mambo hayo mioyoni mwenu?" Yesu alifahamu mawazo yao. Nasi tunasoma katika Maandiko ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na pia imeandikwa kwamba, "Walipo wawili watatu wamekusanyika pamoja, nitakuwa hapo miongoni mwao." Kwa hiyo Wewe upo hapa asubuhi ya leo, katika umbo la Roho Mtakatifu, na unajua kila haja iliyo moyoni mwa watu.

11 Ninakuomba, Baba Mungu, ya kwamba utawajibu na kusema, "Imekwisha. Maombi yenu yemejibiwa, na ni—ninawatumia hakikisho siku hii ya kwamba yote mliyoomba yamejaliwa."

12 Mungu, tunawakumbuka hasa wale ambao hawajaokolewa, walioinua mkono wao. Jalia hii iwe ndiyo ile saa watakayompokea Kristo kama Mwokozi wao.

13 Kabla mkutano huu haujamalizika leo, jalia jambo fulani litukie, Bwana, ambalo lingeuleta Uwepo Wako karibu sana na watu hata watajua ya kwamba Yesu yeye yule aliyetembea katika Galilaya amesimama miongoni mwa watu Wake, wapate kuondoka kutoka hapa leo wakiwa na uhakika ule ule kama wa wale waliokuja kutoka Emau wakati ule. Walipokuwa njiani wakirudi, baada ya kutembea pamoja na Yeye siku nzima, wakizungumza Naye, na Yeye akizungumza nao, na hata hivyo hawakujua sana kwamba alikuwa Ndiye.

14 Ee Mungu, mara nyingi sana sisi tuko namna hiyo. Wewe hunena nasi katika machweo ya jua, katika kuimba kwa ndege, katika mchachariko wa majani, katika kuchanua kwa maua, katika nyimbo za kanisa, nasi hatutambui sana kwamba ni Wewe. Katika vyumba vya wagonjwa hospitalini, mahali pengine pengi, Wewe hunena nasi wala hatutambui sana kwamba ni Wewe.

15 Sasa, Bwana, tunaporudi nyumbani mwetu asubuhi ya leo, tujalie, kama hao walivyofanya, tutambue, tunakuomba Wewe ufanye jambo fulani leo miongoni mwetu kama ulivyotenda huko nyuma. Walijua jambo ulilofanya huko mbele zao. Ulilifanya kabla ya kusulubishwa Kwako, nao walijua ya kwamba huyo alikuwa ni Bwana aliyefufuka. Walirudi kwenye makundi yao, wakishangilia na kumsifu Mungu, kwa kuwa walijua ya kwamba Yeye alikuwa hai. Nao wakasema, "Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi njiani?" Bwana, kuonekana Kwako pale na kufanya kitu kama ulichofanya kabla ya kusulubishwa Kwako, kulithibitisha kufufuka Kwako, ya kwamba Wewe ulikuwa ni Yesu yeye yule, ambaye uliwafanya wakumbuke mazungumzo yote na Wewe. Umezungumza nasi juma zima, Bwana. Sasa onekana miongoni mwetu na ujijulishe kwa kila moyo mhitaji. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

16 [Dada fulani anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mmoja anatoa ufasiri—Mh.]

17 Sasa kusanyiko litaomba. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaomba pamoja—Mh.]: Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe. Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani, kama huko Mbinguni. Utupe leo riziki yetu ya kila siku. Na utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wale watukoseao. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, milele. Amina.

18 Laiti kalamu yangu ingalikuwa ni kifaa cha mchongaji na karatasi yangu iwe jiwe gumu sana, nayo Maneno haya nisemayo sasa, yachongwe juu ya hili yapate kwenda kwa watu wote.

19 Roho Mtakatifu wa Mungu ana njia za ajabu za kuwashughulikia watu Wake. Mara nyingi kupitia maajabu

na kwa karama na miito, ambayo haina majuto, ambayo Mungu huwapa watu Wake kwa neema Yake.

20 Niko nyumbani sasa, kidogo kwa likizo dogo. Kwa kawaida mimi huutumia wakati huu nyumbani, kwenye wakati huu wa mwaka, maana ninapenda kupumzika ninapoenda kuwinda kuchakulo. Nami nimekuwa huko Kentucky pamoja na marafiki wangu juma hili, tukiwinda kuchakulo, mahali nipapendapo sana. Kwa namna fulani nilivunjika moyo, si hasa kwa sababu nisingeweza kuwapata kuchakulo, bali nilijisikia tu kuvunjika moyo. Kitu fulani kilikuwa kikiniambia sina budi kurudi nyumbani. Nami nililala kwenye gari wakati nikirudi.

21 Mwaka jana, kama ninyi nyote mjuavyo, ambayo yameandikwa na pia yamo kwenye ushuhuda na katika kanda. Nilikuwa nimeketi mahali fulani hapa Indiana mahali ambapo Bwana alishuka na kunena nami, kwamba, huduma yangu ya pili, ambayo ilikuwa tayari kutukia hivi karibu sana. Na kuchakulo watatu walinenwa na wakatokea. Ninyi nyote mnaijua hadithi hiyo, nina hakika. Kwa namna fulani, nikipanda juu barabarani nilininii . . . wakati nikiwaachilia hao wavulana wengine waondoke, nikienda kuwinda, ni—nilijisikia visivyo kawaida kwenda mahali hapa tena. Ilikuwa ni kabla ya mapambazuko, ikinyesha, na hata sikujua kama wangeweza kuwinda ama wasingeweza, bali kwamba ningeenda huko kondeni kule. *Kuwinda* maana yake "kuwa peke yako, kuomba." Ndipo nikasimamisha gari nikatoka na kuvuka barabara nikaingia mwituni, na kabla tu hakujapambazuka, kidogo kuna ukungu, mapambazuko.

22 Nilikuwa nimesimama na nikaomba kidogo, kama kawaida, na kumwambia Baba, ya kwamba, "Kile tu ninachohitaji, anijalie." Siamini katika kutumia chochote vibaya, ama kuangamiza; kamwe sijampiga ndege risasi kwa mazoezi ya kulenga shabaha, au chochote kile. Kile niwindacho, mimi hula, ama nampa mtu fulani anayekila. Siamini katika kutumia vibaya chochote. Siamini katika kufanya mambo hayo, kwa maana sio sawa.

23 Ndipo nilipogeuka na nikaanza kupitia kwenye njia ndogo ya miguu niliyoijua karibu na malisho iliyovuka ikaingia kwenye muundo wa L mwituni, ndipo jambo lisilo la kawaida likatukia. Katika matukio yangu yote, sijawahi kuwa na jambo kama hilo. Niliangalia juu ya kilima mkono wangu wa kushoto kutoka mahali nilipokuwa nimesimama, na hapo, zikaja pinde tatu za mvua, zikitokea kwenye kitu kama juu ya kilima. Nazo zilikuwa na urefu kama wa futi thelathini kwenda juu. Kwanza, niliangalia nikaona Nuru ile ndipo nikarudi tu, kwa kuwa nilidhani huenda ikawa ni jua likichomoza. Katika wazo lingine, hazikutokea upande wa jua, zilitokea kusini. Na jambo lingine, kulikuwa ni laini, kuna mawingu, mvua, ikiyesha kila mahali. Hiyo ilikuwa ni Agosti ishirini na tano, Ijumaa iliyopita asubuhi,

nanyi mnajua kulivyokuwa kukinyesha. Na ni mawingu laini kila mahali.

24 Ndipo nikaangalia tena. Nazo hizo hapo, zikiendelea kuwa ndefu zaidi na zaidi, pinde tatu za mvua. Nikatoa kofia yangu. Nikailaza bunduki yangu chini. Nikaanza kuzikaribia huku nimeinua mikono yangu. Kitu fulani kilionekana tu kuniambia, "Umesogea karibu vya kutosha." Nilikuwa nikitaka kuketi chini na kuvua buti zangu nilizokuwa nimevaa, nione kama ningeweza kusogea karibu zaidi. Lakini nilifikia yadi chache kutoka kwake na kuona rangi yake, umefunika kama ukungu unaosogea-sogea. Nikasimama kimya kwa dakika chache. Ulikuwa ukitoka moja kwa moja juu ya mlima mdogo. Nami nikaangalia, wakati hizo tatu (mmoja mkono wa kulia, mmoja wa kushoto, na mmoja katikati) zikishuka mbio na kuingia kwenye kitu kama bakuli. Chochote kile ulichokuwa, ulikuwa hai, Ulikuwa ukisogea na kufanya misogeo yake. Nami nikasimama pale wakati tu ukungu ulipokuwa ukiingia, mapambazuko.

25 Nikageuka na kuangalia tena, nami nikasema kwa sauti kuu, "Ee Mungu, ungetaka mtumishi Wako ajue nini?"

26 Papo hapo Roho wa Bwana akaingia na kusema, "Yesu wa Agano Jipya Ndiye Yehova wa la Kale, Yeye alibadilisha tu kinyago Chake kutoka kwa Roho akawa Mwanadamu." Huko kulikuwa ni kuthibitisha, hakika, Ujumbe wangu kumhusu Yeye. Akinijulisha, kwa hakika ya kwamba miaka hii thelathini na moja haijakuwa ni bure.

27 Nilipoanza kujongea, Huo ulianza kuondoka, nao ukashuka kwenye hiki kitu kama bakuli, kisha ukatoweka. Nikasogea karibu. Niliogopa kwenda karibu zaidi, kwa maana Yeye alikuwa amenisimamisha kabla sijafika pale.

28 Nikageuka na kuona ya kwamba hiyo Nuru, jinsi ambavyo ilikuwa ikiniangazia, ilikuwa imeulenga kabisa ule mti mahali nilipoketi mwaka jana, ambapo wale kuchakulo walitokea. Dakika thelathini na tano ama arobaini baadaye, nilishuka nikapitia mwituni na kuvuka chini ya kile kijito na kadhalika, mpaka nikafikia kwenye mti huu unaotengana katika pande nne (mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini), matawi manne ya huo mti, yaliyochomoza. Nami nikapanda kwenye tawi hili, nikaketi mahali nilipokuwa wakati Yeye aliponiambia juu ya lile Andiko, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka.'" Basi niliposimama pale kidogo, bila kufikiria bado juu ya upinde ule wa mvua, nilikuwa nimeusahau. Nikasimama pale. Na huu umekuwa ni mwaka mbaya sana wa kuwinda kuchakulo, kila kitu kimechelewa, hamna kuchakulo.

29 Nikawazia, "Papa hapa ndipo Mungu aliponipa wale kuchakulo mwaka jana, kuwanena wakawa." Nikaivua kofia yangu tena, ndipo nikasema, "Bwana Mungu, Wewe ungali ni Yesu yeye yule. Ungali ni Mungu."

30 Ndipo kitu Fulani kikaniambia, "Unataka wangapi wakati huu?"

31 Nikasema, "Kama tu nilivyofanya wakati ule mwingine, kiwango cha mwisho." Na kisha nikasema, "Nitapata kiwango hiki cha mwisho kabla ya saa nne leo." Na inavyoonekana isiyo ya kawaida, wakati uo huo nilikuwa katika eneo baya sana la mbu, ambapo palijaa mbu, na kidogo ni eneo la majimaji, ndipo mbu mkubwa mno akaja kuniuma karibu sana na jicho, nami nikasema, "Hakuna mmoja wa hao atakayenisumbua leo hii," nikiwa sina dawa ya kuwafukuzia wala chochote kile. Na, bila kufikiria, nikasema, "Jua litawaka katika dakika thelathini."

32 Na kabla sijamaliza kusema hilo, papo hapo nyuma yangu, kuchakulo aliyefanana kabisa na yule wa mwaka jana, mchanga, mwekundu, aliruka kwenye tawi umbali wa yapata yadi sabini na akaanza kubweka. Nikageuka. Kwenye umbali huo mkubwa, ilikuwa ni vigumu kwangu, kupitia kwa darubini yenye nguvu, kuliona jicho lake. Nikamtupia tu risasi, hivyo tu, hata sikumlenga, si zaidi ya kuielekeza juu ya kuchakulo huyo. Nayo risasi kabisa ikalipiga jicho mahali pale ilipokuwa wakati ule mwingine.

33 Moja kwa moja nikapita humo mwituni. Na dakika tatu kamili kabla ya saa nne, nikampiga risasi kuchakulo wangu wa tatu, kama tu ilivyokuwa mwaka jana, vivyo hivyo hasa. Saa nne kasoro dakika tatu. Mungu, akiwa ni Hakimu wangu mtukufu, hamna hata mbu mmoja aliyelia siku nzima, papo hapo ambapo pana tani nyingi zao, nadhani, kama wangaliweza kupimwa. Na kamwe sikumwona wala kumsikia mmoja. Nilikuwa nikiwasikiliza, nione kama ningeweza. Nami nikasikia sauti, nikawazia, "Huyo hapo mmoja mahali fulani," nami nikasikiliza na ilikuwa ni lori, huko nyuma kabisa kwenye barabara kuu. Na dakika thelathini kamili kutoka wakati huo, jua likaangaza vizuri na angavu.

34 Ndipo nikarudi mahali hapo. Nami nilikuwa nikiwazia, wakati niliposema "kiwango cha mwisho," hilo lilimaanisha *kuchakulo watano*, ambacho ndicho kiwango cha mwisho Indiana. Lakini ninakumbuka mwaka jana, wakati Yeye aliponiuliza inachukua wangapi kwa mlo wangu, nilisema, "watatu," nami nikapata tu watatu. Kwa hiyo jana nilirudi, nilikuwa nikienda mahali pale pale tena, ndipo kitu Fulani kikasema, "Usiende. Vuka barabara."

35 Na kwenye saa nne kamili, juu ya alama, saa nne kwa saa yangu, nikapiga risasi kikomo cha Indiana, kuchakulo wa tano. Ninawatakeni mwone kulikuwako na pinde tatu za mvua, na kulikuwako na mambo matatu yaliyosemwa, kuchakulo watatu waliopatikana. Kulikuwako na mambo matatu: kuchakulo watatu ifikapo saa nne, hamna mbu, jua lingewaka katika dakika thelathini. Na kulikuwako na watatu wa kushuhudia

jambo hilo: Ndugu Banks Wood, mwanangu Billy Paul, na mwanawe David, kutoa ushuhuda wake.

36 Nilipoziona hizo pinde za mvua, karibu upana wa ile duara ya mwangaza ilivyo, yule Malaika wa Bwana, lakini kulikuwako na hao watatu wakijumuika katika Mmoja. Loo, jinsi lilivyousaidia moyo wangu, kujua ya kwamba Mungu, Yesu si mwanadamu tu kama watu wanavyowazia alivyo, nabii tu, kama wazo hili la kisasa leo hii linavyowazia kwamba Yesu ni nabii tu, Yeye ni Yehova wa Agano la Kale aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Na, pale, hilo hakika lilinifariji. Halafu, nikiwazia juu ya somo hilo, ya kwamba Mungu alikuwa amewatafuta watu wengi sana.

37 Sasa, lipo kundi la watu, linalojiita "Umoja" ama "Yesu Pekee." Sikubaliani nao juu ya nadharia yao. Wala sikubaliani—sikubaliani na lile kundi la utatu linalosema ya kwamba kuna Miungu watatu mbalimbali, utatu uliokithiri. Bali ninaamini ya kwamba watatu hao, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ni Mmoja, ya kwamba hizo ni ofisi tatu za Mungu mmoja. Yeye aliishi katika Ubaba, katika Nguzo ya Moto; aliishi katika Uwana, katika Yesu Kristo; na sasa Yeye anaishi katika Roho Mtakatifu, katika Kanisa Lake. Bwana Yesu yeye yule aliyefanyika mwili akakaa kwetu, yuko pamoja nasi leo hii, miongoni mwetu, katika umbo la Roho Mtakatifu.

38 Kati ya matukio yote! Wakati nilipogeuka na kuona Hilo kwa mara ya kwanza, nikiwazia kwanza ingeweza kuwa ni jua likipenya kupitia kwa—kwa wingu mahali fulani, bali ilikuwa ni kabla ya wakati wa jua. Ndipo nilipogeuka tena, na kuona haikuwa ni nuru, ilikuwa ni pinde za mvua. Na halafu wakati nilipoangalia na kuona jambo hilo, nikaingia ganzi mwili mzima.

39 Mtu fulani aliniambia tu, "Je! hukujisikia kupiga mayowe?" La, sikujisikia kupiga mayowe. Matukio hayo kamwe hayakufanyi kujisikia kupiga mayowe, yanakufanya tu ujisikie kutiwa nanga, ambapo tu unajua ya kwamba kuna kitu kinachokwambia, hisi tu ya kuridhika.

40 Sasa, mambo hayo ni kweli. Ninajua tuna mambo yanayosemwa, ambayo mara nyingi baadhi ya watu husema, "Loo, siamini upuuzi kama huo." Siwezi kudhamini hilo, sijui. Ninaweza tu kudhamini kile ninachojua ni kweli. Naye Mungu Mwenyezi, ambaye aliiandika Biblia hii, nami ni mtumishi Wake, Yeye anajua ya kwamba hiyo ni kweli.

41 Wazia hilo, ya kwamba siku tunayoishi, kabla tu ya kuja kwa Bwana, Yesu alisema, "Kutakuwako na ishara angani na duniani, matukio ya kutisha, vimondo virukavyo, makombora, mshangao wa wakati, dhiki kati ya mataifa, na mambo ya kutisha juu ya nchi." Nasi tunaishi katika siku hiyo, kuyaona mambo hayo.

42 Sasa, kwa ajili ya Ujumbe asubuhi ya leo ambao nimeuchagua, ninawatakeni mfungue pamoja nami katika Maandiko, katika Zekaria. Ilikuwa ni ninii yangu. . . Zekaria, m—mlango wa 4.

43 Nilikuwa na shauku ya kuwaambia mambo haya. Mara nyingi mambo mengi hutukia ambayo si—siyaneni, siyasemi. Lakini hili lilikuwa ni la ajabu sana kwangu hata nisingekosa kuliambia kanisa. Halina budi kuelezewa! Na, mbele za Mungu ambaye ninasimama mbele Zake, ni kweli. Ninajua ya kwamba Mungu yupo, nami ninajua ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Imanueli, akiishi miongoni mwa watu Wake leo hii katika umbo la Roho Mtakatifu. Nami ninajua ya kwamba kule Kuja kwa Bwana kunakaribia, wakati ishara na maajabu yanapotokea.

44 Ndio kwanza tuzipitie zile Nyakati Saba za Kanisa, nasi tukajifunza kwamba tuko kwenye Wakati wa mwisho na Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati kanisa lingekuwa lisilojali, lingekuwa baridi, liunde madhehebu, na kujifanyia utaratibu; madhehebu yangelitawala, yalile. Lakini ahadi kwamba kungekuwako na masalio waliosalia. Kungekuwako na Kanisa litakalotawanyika kila mahali, bali Mungu angelikusanya pamoja na kulinyakua Utukufuni; maskini kundi dogo lililotakaswa mahali fulani, likimngojea Bwana.

45 Ndipo hivi majuzi nilipoyachukua *Majuma Sabini Ya Danieli*, nikisimama papa hapa mimbarani, kitu Fulani kilinigusa, kamwe sijaweza kuliacha. Kuona saa tunayoishi! Ninataka kwenda mahali fulani na kufanya jambo lingine, kuliondoa moyoni mwangu. Nina wapendwa wengi mno ambao hawajaokolewa. Nikijua, nifanye nini kuwafanya waokolewe? Ninaweza kufanya nini? Nimeihubiri Injili. Mungu amefanya ishara kuu na maajabu kuliko yale amewahi kufanya tangu ulimwengu, tangu siku za Bwana Yesu, hajapata kuzifanya katika historia yote ya wakati. Na imezunguka kote ulimwenguni. Na hata hivyo ulimwengu unaendelea kuwa mbaya zaidi. Lakini hata hivyo inanibidi kukumbuka ya kwamba tunaishi kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia, ambako watakuwa wabaya zaidi, Nalo lilisema watakuwa hivyo.

46 Ndipo nikachagua asubuhi ya leo, kwa kuwa huo Ujumbe ulishambuliwa sana, jambo lingine ambalo ninafuatiliwa sana kulihusu, ni, kuihubiri neema. Ninataka kuizungumzia hiyo asubuhi ya leo ninaposoma mlango wa 4 wa Zekaria, sehemu yake.

> *Na yule malaika aliyesema nami akanijia mara ya pili,* akaniamsha, *kama mtu aamshwavyo katika. . . usingizi.*
>
> *Na* Yeye *akaniuliza, Unaona nini? Nikasema, Nimeangalia, na tazama, kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake, na taa zake saba juu*

yake; tena iko mirija saba ya kuleta mafuta kwa taa zote zilizo juu yake.

Na mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume wa lile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto.

Nami nikajibu, nikamwambia yule malaika aliyesema nami, nikasema, Ee Bwana wangu, vitu hivi ni nini?

Ndipo malaika aliyesema nami akajibu, akaniambia, Hujui vitu hivi ni nini? Nikasema, La, Bwana wangu.

Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho wangu, asema BWANA wa majeshi.

47 Mnaona? Ujumbe hautakuja kwa uwezo mwingi wala nguvu, bali kwa Roho wa Mungu! Kifungu cha mwisho, kifungu cha 7.

Nani wewe, Ee mlima mkubwa, mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare; naye atalileta lile jiwe la kuwekea juu kabisa, pamoja na vigelegele *vya Neema, neema, ilikalie. Neema, neema, ilikalie.*

48 Sote tunayafahamu Maandiko haya, ambao husoma Biblia. Tunajua huu ulikuwa ni ule wakati wa maandalizi ya kurejeshwa upya kwa hekalu. Naye Zerubabeli alikuwa ni mtawala mkuu miongoni mwa watu, ambaye alikuwa ameweka msingi wa jengo hilo. Sasa, ninyi, ninawatakeni mvae mawazo yenu ya kiroho, jaketi ya upako, asubuhi ya leo, tunapowazia. Naye huyu mtawala mkuu alikuwa ameyakinia kuijenga upya nyumba ya Bwana. Halafu basi, alipofanya hivyo, alikuwa ameweka jiwe la msingi.

49 Na tunapoendelea kusoma zaidi, tunaona ya kwamba Mungu alisema, "Zerubabeli ameuweka msingi kwa mikono yake, pia yeye atalileta jiwe la kuwekea juu kabisa." Ninawatakeni mwone, kamwe Yeye hakusema ataleta "Jiwe la Pembeni." Yeye ataleta "jiwe la kuwekwa juu kabisa."

50 Nasi tunajua ya kwamba Maandiko yanasema ya kwamba Yesu Ndiye lile Jiwe Kuu la Pembeni, na pia Ndiye lile Jiwe la Kuwekwa Juu Kabisa. Sasa kama tutawazia kwa dakika chache, ya kwamba, yule mjumbe wa saba wa kanisa alikuwa "airudishe Imani ya watoto iwaelekee baba zao." Kwa maneno mengine, kulijenga Kanisa tena chini ya Nguvu za Roho. "Si kwa nguvu, wala kwa uwezo, bali kwa Roho Wangu," asema Bwana. Si kwa shirika, wala kwa dhehebu, bali kwa Roho Mtakatifu, Mungu atalileta Kanisa katika siku ya mwisho.

51 Zerubabeli, yule mtawala pamoja na Yoshua, ndiye aliyekuwa alete hili jiwe la kuwekwa juu kabisa. Alikuwa ameweka msingi, alikuwa amewarudisha watu kwenye ule msingi, katika mfano.

52 Ambapo, sote tunajua ya kwamba hii minara ya taa na kadhalika iliwakilisha Wayahudi na kanisa pia. Ilikuwa ni "matawi ya mzeituni," Biblia ilisema hapa. Na tawi la mzeituni, sisi ni tawi mwitu ambalo lilipandikizwa kwenye shina la mzeituni wa asili; Mataifa! Na kutoka kwenye matawi haya mawili inatokea mirija ya chetezo, ikiingia kwenye vile vinara saba vya dhahabu, kuziangazia Nuru zile Nyakati Saba za Kanisa.

53 Sasa kumbukeni, katika mafundisho yetu kwenye masomo ambayo ndiyo kwanza tupitie, ya kwamba tulichukua piramidi ile kuu na kuisoma kwa kitambo kidogo, ambayo hapana budi ilijengwa na Henoko. Nalo jiwe la kifuniko halikuwekwa kwenye piramidi hiyo. Nimekuwa huko. Usanifu wa ujenzi wake kamwe hauna mbadala hata wa leo. Hatuna mitambo ambayo ingeweza kujenga piramidi, hakuna nguvu (ila ziwe ni nguvu za atomiki) ambazo zingeweza kuijenga piramidi, kwa kuwa ni kubwa mno. Mawe ambayo yangekuwa na uzito wa matani na matani na matani, yanasimama huko juu sana hewani, yameunganishwa kwa ustadi sana hata wembe mwembamba usingeweza . . . Nayo hayajatiwa sementi, yamekatwa tu kusudi yashikane.

54 Hivyo ndivyo mwili wa Yesu Kristo unavyopaswa kuwa, kukatwa vizuri sana na Roho Mtakatifu, kwa Chombo kikuu cha Mungu na Kifaa, tupate kuunganishwa kama Mtu mmoja. Hatujagawanyika. Inatupasa kuwa Mtu mmoja! Na inaonyesha ya kwamba hakuna mtambo unaoweza kufanya jambo hilo hivyo. Inahitaji Mungu kufanya hivyo. Hakuna mitambo ya madhehebu, hakuna vyama, hakuna kimoja cha vitu hivi kinachoweza kufanya hivyo, hata viwe na makusudio mazuri jinsi gani. Kamwe haviwezi kulifanya, kwa kuwa inahitaji Mungu kufanya jambo hili, Roho Mtakatifu.

55 Sidhani nina noti ya dola mfukoni mwangu. Lakini kuna . . . Naam, ninayo, nina noti ya dola. Samahani. Nyuma ya noti hii ya dola utaona ule muhuri wa Marekani mkono wa kushoto, kuwaelekea ninyi. Kutoka kwangu, ingekuwa ni mkono wa kushoto; kwenu, ni wa kulia. Ni tai. Na pia mle ndani nembo na kadhalika. Lakini upande *huu* hapa, mkono wa kulia, kwangu, mnaona piramidi. Na mnaona, juu ya piramidi kuna jiwe la kifuniko, na chini ya hapo inasema, "Muhuri Mkuu." Hata kwenye sarafu yetu, ambayo inatubidi kutambua. Hakuna kafiri anayeweza kuuondolea mbali Ukristo. Kila barua unayoiandikia tarehe, inaonyesha siku ya kuzaliwa kwa Bwana wetu. Kila kalenda, kila kitu kinanena habari Zake. Na hata kwenye sarafu yetu, Jiwe la Kuwekwa Juu Kabisa, ambalo ni Kristo! Ni kwa nini hawakuweka jiwe la kuwekwa juu kabisa juu ya piramidi? Kwa sababu lile Jiwe la Kuwekea Juu Kabisa lilikataliwa wakati lilipokuja.

56 Lakini sasa, kulingana na unabii, Jiwe la Kuwekwa Juu Kabisa litakuja. Nami nawatakeni mwone ya kwamba, Jiwe

la Kuwekwa Juu Kabisa litakapokuja, yule mtawala ambaye atautangaza Ujumbe atalia "Neema! Neema!" Kwa kuwa tunaokolewa kwa neema, hiyo si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Nao Ujumbe wa neema umekanyagwa chini ya miguu ya watu mpaka umekuwa ni fedheha. Wengine wao wanakimbilia kwenye usalama wa Milele, wengine wanakimbia wanaingilia kwenye kila kitu. Lakini, Ujumbe wa kweli wa neema unabaki vile vile, na hapo ndipo Shetani anapojaribu kuutoa Kanisani. Lakini neema ya Mungu ndiyo sote tumeokolewa kwayo.

57 Kwa hiyo katika Uungu wa Yesu Kristo, kama Bwana Mungu angekuja pale na kuthibitisha ya kwamba hiyo ni Kweli, si hivyo tu, bali kwa Neno Lake anathibitisha kwamba ni Kweli, na kwa ishara na maajabu anathibitisha ni Kweli, basi, pia, neema ni Kweli. Basi kwa nini mtu yeyote akosoe na kusema ya kwamba neema si ya kweli, ya kwamba "tunaokolewa kwa matendo"? Tunaokolewa kwa neema, hiyo ni kwa imani, sio kwa matendo. Matendo yanaonyesha ya kwamba umeokolewa. Lakini kinachokuokoa ni neema ya Mungu. Neema inakuokoa. Neema ni yale Mungu anayokutendea. Matendo ni yale unayomtendea Mungu, kuonyesha shukrani kwa yale Mungu aliyokufanyia. Lakini unaokolewa kwa neema!

58 Baadhi ya watu wanawazia, "Kwa sababu ninaenda kujiunga na kanisa, na kuandika jina langu kwenye kitabu, hilo tu ndilo linalonibidi kufanya." Watu wengine wanawazia, "Kwa kuwa mimi hupaza sauti, hilo tu ndilo linalonipasa kufanya." Wengine wanawazia, "Kwa kuwa mimi hunena kwa lugha, hilo tu ndilo linalonipasa kufanya." Wengine wanawazia, "Kwa kuwa nina nguvu za kuwaponya wagonjwa, hilo tu ndilo linalonipasa kufanya." Sivyo! Ni neema ya Mungu ndiyo inayokuokoa, Neema ya ajabu ya Mungu. Siwezi kutegemea ustahilifu wowote. Wengine walisema, "Vema, huyo hapo mtu mkuu. Mtu huyo, nimemsikia akisimama na kufanya *hili*, nimemsikia akisimama na kufanya *lile*."

59 Paulo alisema, katika Wakorintho wa Kwanza 13, "Nijaposema kwa lugha ya wanadamu na Malaika, nijapokuwa na utambuzi, nijapokuwa na karama, kuwalisha, nitachukua mali yangu yote kuwalisha maskini, nijapoihamisha milima kwa imani, nijapokuwa na maarifa kufahamu mambo yote, si kitu mimi mpaka upendo utakapoingia, ambao ni neema." Mungu hana budi kufanya hilo. Unaweza kufanya mambo haya yote na bado upotee. Neema ndiyo inayokuokoa, neema ya Mungu kwa jamii ya binadamu.

60 Kuwaza kumhusu Yeye! Nilikuwa nikiwazia juu ya hiyo neema mara baada ya hilo kutukia Ijumaa asubuhi, kwenye mapambazuko, huko juu kwenye lile konde wakati nilipoketi kwenye gogo, baadaye, nayo machozi yakatiririka machoni mwangu. "Ee, Mungu, neema Yako imeinama kuniokoa. Kwa

nini ulimhurumia hivi maskini mwovu kama mimi, asiye na elimu? Ulipataje kushuka kwenye maskini maskani yetu ndogo, ambapo amani, na watu wenye hadhi duni ya maisha, maskini, hawana kitu humu ulimwenguni, na hata hivyo neema yako imemiminwa mioyoni mwetu, na Roho Mtakatifu, hata unayaponya magonjwa yetu na kuziokoa dhambi zetu, unatuokoa na dhambi zetu, hasa, na kutufanya watu Wako, kutushughulikia?"

61 Ndipo nikawaza juu ya Daudi, jinsi ambavyo wakati alipowazia kumjengea Bwana nyumba, alisema, "Si vizuri kwangu kuishi katika nyumba ya mwerezi, nalo Sanduku la agano la Mungu wangu chini ya ngozi za kondoo na maskani."

62 Mungu akamwambia nabii, "Nenda ukamwambie mtumishi Wangu, Daudi, nilimtoa katika zizi la kondoo, kutoka kwenye kuwalisha hao kondoo wachache huko nje wa baba yake, na 'kukufanyia jina kuu kama watu wakuu duniani.'"

63 Niliwazia juu ya neema ya Mungu, jinsi ambavyo Yeye angefanya jambo hilo, kuokoa hata wa chini kabisa! Halafu angemchukua maskini mwovu kama mimi, na kunipa nafasi ya kuihubiri Injili na kuwaona wengine wakiokolewa, kuwaona wakiponywa; kuona nyumba ambazo zimevunjika, zikinyoshwa tena; kuona maisha ambayo yameangamizwa, yakinyoshwa tena. Na kunipa neema! Nikawazia, "Loo, ni neema ya ajabu!" Halafu kumjia maskini mwinda kuchakulo duni huko mwituni, mwenye hadhi ya chini, na kujifanya katika mfano wa *upinde wa mvua*, ambao unamaanisha "agano," pamoja na Ujumbe alionipa kuuhubiri, na kuufanya pale katika agano, ya kwamba Yeye yuko nyuma Yake! Naye atakuwa nyuma Yake, kwa kuwa Ujumbe ni wa Yesu Kristo na utukufu Wake.

64 Jinsi ambavyo ameniruhusu kwenda kote ulimwenguni, kuuzunguka ulimwengu, kwa mataifa, kwa mamilioni ya watu, nikawaona mamilioni wakija kwa Bwana na kumkubali kama Mwokozi wao, nikawaona wamejazwa na wema Wake na kutakaswa kwa nguvu Zake, nikawaona wameponywa na nguvu Zake kuu. Basi ninaweza kulia kama yule nabii, na kusema, "Si kwa nguvu, wala kwa uwezo, bali ni kwa Roho wa Mungu." Si kwa elimu, wala kwa theolojia, bali kwa Roho wa Mungu Yeye anawaokoa watu. Kwa Roho wa Mungu anawaponya watu. Ni Roho wa Mungu ndiye anawapa watu Ujumbe. Roho wa Mungu Ndiye anayelithibitisha Neno.

65 Tunao wanatheolojia siku hizi, tuna Madaktari wa Uungu, tuna watu mashuhuri kote ulimwenguni, ambao ni werevu, wenye akili na wana elimu. Lakini inachukua urahisi wa kumwamini Mungu, kulifanya Neno Lake linene, kuonyesha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Inahitaji moyo mnyenyekevu uliojitolea kwa Mungu, kumleta Yesu Kristo katika wakati uliopo. Amina! Kama ingalihitaji

theolojia, vipi Mpresbiteri, Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, na kadhalika; tusingekuwa na nafasi, sisi maskini watu wasio na elimu. Lakini haihitaji maarifa. “Si kwa nguvu wala uwezo, bali kwa Roho Wangu,” asema Mungu, “Nitaifunua siri hii.” Na, “Yeye ataililia, Neema, neema, pamoja na makelele na vilio.” Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, neema ya ajabu ya Mungu kwa watu Wake. Jinsi anavyomchukua mtu asiye na elimu, asiye na kisomo, kuonyesha ya kwamba Yesu ni yeye yule.

66 Wakati alipokuja, Yeye kamwe hakuwajia wanatheolojia wakuu. Wala hakuenda kwa Kayafa, kuhani mkuu; akajikuta tu amehukumiwa naye.

67 Bali aliwachukua wavuvi, watu waliokuwa maskini na walioishi maisha ya kawaida. Na hapo Yeye akajifunua Mwenyewe, na kusema, “Nifuateni, nami nitawafanya wavuvi wa watu,” kuonyesha ya kwamba neema Yake ingali ilishuka kutoka kwa Wayahudi ikawaendea Mataifa, kuwaita watu kwa ajili ya Jina Lake katika siku hizi za mwisho, kama tulivyoyapitia hivi karibuni. Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu!

68 Neema ni ya kale. Neema ni ya zamani za kale kama ulimwengu ulivyo. Neema ilionyeshwa kwa jamii ya mwanadamu kwa mara ya kwanza wakati tulipokuwa na mwanzo wa jamii ya mwanadamu. Wakati jamii ya binadamu ilipoumbwa kwa mara ya kwanza katika bustani ya Edeni, kwenye ile asubuhi yenye giza wakati maskini mwanamke yule aliyevuka mstari wa utengano, na alikuwa amezikiuka amri za Mungu na kumshawishi mumewe kufanya jambo lile lile, ndipo sheria ilipovunjwa. Sheria haina budi kuwa na adhabu la sivyo si sheria. Nayo sheria hiyo ilikuwa, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.”

69 Kumbukeni, kiti cha kwanza cha hukumu kilikuwa duniani, nacho kilikuwa katika bustani ya Edeni. Nacho kiti cha mwisho cha hukumu kitakuwa juu ya dunia, wakati wa mwisho, Kiti Cheupe cha Enzi.

70 Lakini wakati Yehova aliposhuka, ningeweza kuwazia hata hakukuwako na nyota ya kutoa mwanga, ilikuwa giza sana katika bustani hiyo ndogo ya nuru ambayo wakati mmoja ilikuwa, kwa sababu dhambi ilikuwa imeifutilia mbali, ilikuwa imeiondoa Nuru kutoka miongoni mwao.

71 Hiyo ndiyo shida ya makanisa leo. Hiyo ndiyo shida ya watu leo hii. Dhambi imeifutilia mbali Nuru ya Mungu aliye hai, kuonyesha ya kwamba Kristo angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye yu hai kuokoa kabisa, na kumponya mgonjwa, aliye duni sana.

72 Loo, jinsi lilivyokuwa ni jambo la kutisha sana asubuhi hiyo, giza likining’inia bustanini! Nitawazia ukungu wa nguo za magunia. Ningewazia kila jani halikusogea kamwe. Upepo

haukutikisa. Lilikuwa giza na kutisha sana, kwa kuwa dhambi ilikuwa imefutilia mbali.

73 Huyu hapa Yehova anakuja kama ngurumo ya radi, akitembea bustanini, akilia, "Adamu, uko wapi?" Hapo ndipo Adamu alipotambua alikuwa uchi na alikuwa ametenda dhambi mbele za Mungu. Alijificha na akajaribu kujifanyia dini fulani, bali haikufaa kitu. Mungu aliwaua kondoo wachache, akachukua ngozi, na kuonyesha ya kwamba ilibidi kitu fulani kufa kuifunika dhambi.

74 Kujiunga na kanisa kamwe hakutaifunika dhambi. Hakuna maungamo ya jicho kavu yatakayoifunika dhambi. Inahitaji huzuni na toba, na neema ya Mungu, kuifunika dhambi; kwa kuwa Damu ya Yesu Kristo, Yule ambaye Mungu alimwua pale Kalvari, kuifunika dhambi.

75 Pale bustanini asubuhi hiyo, wakati dhambi ilikuwa ni nyeusi sana, Yehova aliingia. Pale walisimama mume na mke Wake, wamehukumiwa. Hakungekuwako na jamii ya binadamu tena, iliwabidi kufa; mauti juu ya jamii ya binadamu, kuurudisha ulimwengu kwa wanyama wa mwitu na hakungekuwako na jamii ya binadamu tena. Lakini katika saa hiyo yenye giza kuliko zote, kwenye wakati huo ambapo matumaini yote yalikuwa yamekwisha, neema ilikuja ikitiririka pale, kasema, "Nitawapa Mkombozi, Masihi." Loo, ni ajabu jinsi Mungu angeweza kufanya jambo hilo! Neema ya ajabu ya Mungu katika bustani ya Edeni, ambayo iliwapa ahadi ya Mwenye Haki Ambaye angekuja kupitia kwa mwanamke. "Uzao wa mwanamke utakiponda kichwa cha nyoka," mwenye hatia, "nacho kichwa chake kitakiponda kisigino chake," kuonyesha kungekuwako na mateso kwa Kanisa. Lakini Yeye aliahidi ushindi! Ni kitu gani kilichomtoa Mkombozi? Neema!

76 Wangeweza kuonyesha nini kuistahili neema? Wangeonyesha nini kufanya hivyo? Ule msemo wa jeshi, samahani kwake, ninataka tu kuutoa kutoka kwenye mimbara yangu hapa kueleza jambo muhimu, "kulaumiana." Adamu alisema, "Mwanamke uliyenipa Wewe alifanya hilo." Mwanamke akasema, "Nyoka alinidanganya." Mmoja alimlaumu mwenzake. Hapakuwapo na matumaini kwao.

77 Lakini Mungu alitoa neema, nayo ikaingia kwa nguvu! Naye akasema, "Lakini nitaweka njia, kwa namna fulani. Nitawaokoa, haidhuru. Mmekosea, mmekiuka amri Zangu. Nazo amri Zangu hazina budi kusimama, lakini hukumu ya kutokana na sheria Zangu itatolewa. Kwa hiyo itabidi kifo kuwepo, kwa maana Mimi nimesema 'kifo.'"

78 Sasa, rafiki zangu Wakristo. Na kanda hizi hapa zinazorekodiwa zitasambaa ulimwenguni kote. Hebu niwaulize jambo fulani, ninyi mnaojaribu kumfanya Mungu kuwa Miungu

watatu, ama ninyi mnaojaribu kumfanya kuwa ni mmoja, kama kidole chako. Yeye ni mtu mmoja!

79 Isingekuwa ni haki kwa Mungu kumfanya Malaika kufa. Yeye asingekuwa ni Hakimu mzuri na kumfanya Malaika afe kwa ajili ya binadamu. Hilo bado halilitibu, kwa kuwa sheria Yake kuu inahitaji mauti, na kitu fulani hakina budi kufa, na Malaika hawezi kufa. Wala Yeye asingeweza kusema, "Hawa, kwa kuwa umemfanya Adamu kufanya hivi, nitakufanya ufe, nimwache Adamu aishi," kwa sababu Adamu alishiriki pia.

80 Kama vile mtu fulani alivyosema, "Pilato alihesabiwa haki, yeye aliiosha mikono yake." Huwezi kuiosha Damu ya Yesu Kristo itoke mikononi mwako. Kamwe hutaondoka kwenye jengo hili asubuhi ya leo na kwenda Mbinguni, kama ukifa katika dhambi zako. Iko mikononi mwako. Kwa hiyo, hiyo si kweli.

81 Kulikuwako na njia moja tu ya haki. Kuna njia moja tu ingaliwezekana, masharti ya sheria kuu ya Mungu, yangeweza kuzingatiwa. Ilimbidi kuitimiza Yeye Mwenyewe. Ilimbidi kuitimiza. Mungu ni Roho na Yeye hawezi kufa. Kwa hiyo ilimbidi Mungu kufanyika mtu, Naye alikufa katika mwili wa binadamu, katika umbo la mtu aliyeitwa "Yesu Kristo," na Huyo alikuwa Ndiye Masihi aliyeahidiwa aliyeinunua neema. Hapo ndipo unapoona ya kwamba Mungu na Kristo ni Mtu yule yule, Mungu akiishi katika Kristo. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja, Baba Yangu anaishi ndani Yangu; si Mimi ninayenena Neno, bali ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu." Mungu katika Kristo! Hakika.

82 Neema iliahidiwa katika bustani ya Edeni, nayo neema ikaja, neema kwa Adamu na Hawa. Hakuna mahali pa kwenda, hakuna njia ya kugeukia na hata hivyo neema ilifanya njia!

83 Hebu niseme jambo hili, rafiki yangu mwenye dhambi. Huenda ukawa hapa asubuhi ya leo kahaba, huenda ukawa hapa asubuhi ya leo mwandama wanawake, huenda ukawa hapa mlevi ama mcheza kamari, ama mwuaji. Huenda ukawa hapa kama mume mchafu, mke mchafu. Huenda ukawa ndiye mwenye dhambi aliye mchafu kuliko wote. Unasema, "Nimepita kiwango hicho cha ukombozi." La, hujapita, la sivyo usingekuwa kanisani asubuhi ya leo. Neema itakufanyia njia katika saa hii ya giza kama utaikubali. Ilimbidi Adamu kuwa radhi kuipokea, nawe pia. Ikubali.

84 Neema ya Mungu iliunyosha mkono katika wakati wa Nuhu. Nuhu, mtu wa kawaida tu, yeye na familia yake. Lakini kwa sababu Nuhu alimcha Mungu, yeye alimwamini Mungu! Huwezi kumcha Mungu pasipo kuamini. Unawezaje kukicha kitu ambacho hukiamini? Inakubidi kumcha Mungu. Sulemani alisema, "Kumcha Mungu ndio mwanzo wa hekima." Sasa, kumcha Mungu tu, unaanza kuwa na hekima. Na kumcha

Mungu, Nuhu alimcha Bwana na kumwamini Bwana. Na hilo ndilo Mungu analoheshimu, ni imani yako katika Yeye. Hiyo ni kweli. Ndipo wakati uchaji wa Mungu ulipokuja juu ya Nuhu, Mungu alimwita kwa neema, na kumwokoa na nyumba yake kwa sababu neema ndiyo iliyofanya jambo hilo. Si kwa sababu Nuhu alikuwa mtu mkubwa mno mwenye sura nzuri kuliko wengine wote, si kwa sababu Nuhu alienda kwenye kanisa lililo bora kuliko yote yaliyoko nchini, sio kwa sababu alikuwa ni mwanachama wa shirika lililo bora kuliko yote, si kwa sababu alivalia vizuri zaidi, sio kwa sababu alikuwa na fedha nyingi zaidi, sio kwa sababu alikuwa ni mtu fulani maalum. Lakini ni kwa sababu ya neema ya Mungu, Mungu alimwokoa Nuhu. Neema ilimwokoa Nuhu (si matendo yake; bali neema Yake) na pia ikaiokoa familia yake.

85 Tutamtaja mtu mwingine ambaye neema ya Mungu ilimfikia, wengi wao, tutazungumza tu juu ya wachache. Ibrahimu. Ibrahimu, si mtu maalum, alishuka kutoka kwenye mnara wa Babeli, labda alitoka kwenye kundi la waabudu sanamu (baba yake), akashuka kwenye nchi ya Shinari kule chini, apate kuishi katika mji wa Uri. Na wakati akiwa kule, Mungu alinena naye kwa neema. Si kwa sababu alikuwa ni tofauti, si kwa sababu alikuwa ni mtu bora zaidi; bali, kwa neema, Mungu alimwita. Biblia inalieleza hilo dhahiri. Loo, Ibrahimu, jinsi ambavyo Ibrahimu aliijaribu subira ya Mungu! Alimwambia, akasema, "Ibrahimu, kaa katika nchi hii, kamwe usitoke humu." Lakini mara njaa ilipoingia, Ibrahimu akatoroka.

86 Ibrahimu alinena kutuhusu. Mungu alimchukua—Mungu alimchukua Ibrahimu kwa neema, na kumwokoa. Na hivyo ndivyo anavyokuchukua wewe, kwa neema. Nasi tunaijaribu subira yake namna gani? Leo tu juu, kesho tuko chini. Siku moja tunaamini, kesho yake tunashangaa. Leo sisi ni Methodisti, kesho sisi ni Baptisti. Leo tunaamini katika uponyaji wa Kiungu, kesho tumbo linauma nasi hatujui kama tunaamini ama hatuamini. Lakini hata hivyo katikati ya hayo yote, Mungu anatutaka tutulie. Bali anatuokoa, kwa vyovyote vile. Kama isingalikuwa ni neema ya Mungu, sote tungekuwa tumekwisha. Hakika. Mungu hutuokoa kwa neema Yake.

87 Ibrahimu alipaswa kukaa katika nchi hiyo, bali alishuka akaenda huko kwa Wakaldayo, ama, sio Wakaldayo, bali Wafilisti. Alienda kule akawe mgeni, aitoroke njaa. Mambo yalikuwa kidogo ni magumu kwenye nchi yake, kwa hiyo akashuka akaenda kule kuwa mgeni pamoja nao. Akafanya vile hasa Mungu alimwambia asifanye, lakini hata hivyo neema ya Mungu ikamtokea, ikamzuia Farao ku-. . . ama nanii—ama mfalme kumchukua mke wake. Neema ya Mungu. Wakati Ibrahimu aliposema, "Ni dada yangu," akasema uongo juu yake,

lakini hata hivyo neema ya Mungu ilimshikilia kwa sababu alitubu. Alikuwa radhi kutubu.

88 Na yeyote aliye tayari kutubu, neema ya Mungu ingali inakujia. Neema ya Mungu inakutafuta. Kwa hiyo, hiyo inawajia ninyi mliorudi nyuma asubuhi ya leo, neema ya Mungu ingali inakutafuta. Kama utatubu tu, neema ya Mungu inatosha.

89 Jinsi ambavyo alimchukua maskini mzee mwema Ibrahimu, akamrudisha! Pia kumbukeni, Ibrahimu hakuokolewa kwa matendo yake, aliokolewa kwa neema. Ibrahimu aliokolewa kwa imani, ambayo ni neema. Naye Mungu alimwokoa Ibrahimu kwa sababu ya neema Yake, sio kwa sababu ya mwenendo wake. Alimwokoa kwa sababu ya neema Yake. Loo, ni zuri jinsi gani! Aliokolewa kwa neema.

90 Hebu tuwachukue Israeli. Nina Maandiko yaliyoandikwa hapa. Nimeyaandika na ninaweza tu kuyarejea kichwani mwangu. Kama mnataka kuyaandika, hili litakuwa ni zuri kukumbuka mkitaka, Kumbukumbu la Torati 7:7. Mungu alimpa Ibrahimu ahadi Yake, ama hakumpa Ibrahimu, samahani, aliwapa Israeli. Na akawaambia, "Kama hamtajihusisha na ibada za sanamu! Kama hamtafanya mambo haya! Kama mtakaa mbali na sherehe hizi zote za kipagani! Kama mtayafanya mambo haya yote, basi nitawaleta kwenye nchi nzuri, nitawashughulikia, nitawalisha, nitawaongoza. Nitafanya mambo haya kama mtafanya hivi na vile, kama mtanipenda Mimi, kama mtazitimiza Amri Zangu, sheria Zangu, hukumu Zangu. Nitafanya mambo haya yote kama mtafanya tu jambo fulani, na kutimiza Amri Zangu na kunipenda Mimi."

91 Ni kama tu mume akimchukua mke, na kusema, "Kama utakuwa mke mwema, kama utaitunza nyumba, kama utakuwa mwaminifu kwangu, kama utatunza nguo zangu zikiwa safi; kama tukipata watoto, kama utakuwa mama mzuri kwao; kama utafanya mambo, nitafanya kazi mpaka mikono yangu itokwe na damu, kukupa riziki, kama utafanya hivyo." Lakini basi, wazieni, vipi kama mwanamke huyo akiharibika, awe mzembe, hafanyi kazi, hatafanya lolote? Basi inahitaji neema kuiweka familia hiyo pamoja.

92 Ee Mungu! Ilihitaji neema ya Yehova kuiweka familia Yake pamoja. Na hiyo ndiyo njia pekee tulivyo familia ya Yehova leo, ni kwa sababu ya neema ya Yesu Kristo; tungekuwa sote tumekwisha. Lakini ni neema, loo, neema!

93 Sasa, bali hawakuzitii. Lakini walikuwa, kamwe hawakuifikia ahadi kamilifu; sio kizazi hicho. La, wale waliofanyiwa hiyo ahadi, waliangamia nyikani. Lakini Mungu aliwalisha, Mungu aliwashughulikia, Mungu aliwapenda, alitembea huko. Kwa nini? Neema Yake ilifanya hivyo, neema Yake kwa sababu ya ahadi Yake, ahadi Yake wakati huo, neema

iliyoambatana na ahadi Yake. Bali kamwe hawakufikia kwenye manufaa kamili ya nchi ya ahadi.

94 Na wala kanisa hili halifikii manufaa yake kamili. Neema ya Mungu inatushikilia. Lakini Yeye anataka kulipata kanisa litakalomtii, watu watakaolichukua Neno Lake na kusema "Ni Kweli," bila kujali dhehebu lako. Anawataka watu ambao hawatasema, "Vema, mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe. Mimi ni Mpresbiteri, mimi ni Mmethodisti, mimi ni Mkatoliki, mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe." Hiyo siyo neema; hiyo inaonyesha kuna kasoro fulani.

95 Lakini mtu, haidhuru, ambaye atalisoma Neno la Mungu na kuona ya kwamba huna budi kuzaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu, wataamini hilo, watalichukua kwa Neno. Watalichukua Neno jinsi lisemavyo hasa.

96 Kama vile katika mabatizo na kunyunyiziwa; ubatizo ni wa kweli. Hakuna mtu katika Biblia aliyepata kunyunyiziwa, hakuna kitu kama hicho katika Maandiko. Wala kamwe hapakuwa na mtu yeyote aliyebatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," katika Biblia. Wote, kila mmoja wao, walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Kwa hiyo hakuna mmoja, hakuna hata chembe moja ya historia ya . . . Kama mtu yeyote anaweza kuonyesha mahali popote, mahali popote katika historia, ambapo mtu yeyote alipata kubatizwa katika Biblia, ama miaka mia tatu baada ya kifo *cha* mtume wa mwisho, mpaka kufikia kanisa Katoliki, kama mtu yeyote anaweza kuonyesha mahali popote ambapo mtu yeyote alipata kunyunyiziwa ama kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," mpaka kanisa Katoliki, unawajibika kibinafsi kuja kuniambia. Haipo. Lakini tunafanya nini?

97 Tumepitia *Nyakati Za Kanisa* na kuona ambapo iliwabidi kufanya hivyo. Kwa hiyo, mnaona, Mungu anataka mtu atakayemwamini. Kama halipo kwenye Maandiko, basi si mwanadamu . . . ni fundisho la kujibunia wala si Fundisho la Biblia. Mnaona? Kwa hiyo haijalishi kile kanisa lilicho, jinsi umekuwa makosani, hiyo inaleta tofauti gani? Ni jinsi unavyoweza kuwa sahihi sasa! Neema ya Mungu imekuonyesha, basi tembea ndani yake. Neema ya Mungu!

98 Mkumbukeni Musa, pia, yule kiongozi mkuu. Mungu alipaswa kumwua wakati aliposhuka kule kujitukuza mwenyewe kwa kuupiga ule Mwamba, na kusema, "Mnaona yale ninayoweza kufanya?" kwa maneno mengine. "Enyi waasi, hivi ni lazima tuwachotee maji kutoka kwenye huu Mwamba?" Naye akaupiga wala maji hayakutokea; akaupiga tena. Alifanya nini? Alishuhudia juu ya udhaifu wa—wa Kristo, maana Kristo alikuwa ndiye huo Mwamba. Hilo Ndilo Jiwe la Kuwekwa Juu Kabisa. Badala ya kuupiga, ama kunena nao . . .

99 Ulipigwa mara moja. Kumbukeni, Mungu alimwambia Musa katika Kutoka, "Nenda zako Nami nitasimama mbele—mbele zako, juu ya Mwamba, na uupige Mwamba huo." Naye akaupiga Mwamba nao ukatoa maji. Mungu akasema, "Wakati mwingine, nenda ukaseme na Mwamba nao utatoa maji Yake."

100 Lakini Musa alitaka kuonyesha ya kwamba alikuwa na mamlaka kidogo, nguvu kidogo, kwa hiyo akasema, "Nitawaletea maji kutoka kwenye Mwamba huu." Mungu alipaswa kumwua, kwa ajili ya jambo hilo. Mungu alipaswa kumtenganisha, kwa kuwa alivunja sheria ya Mungu papo hapo, maana alinena juu ya udhaifu wa Kristo, inambidi kupigwa mara ya pili. Kristo alipigwa tu mara moja. Sasa tunanena na Mwamba, Nao unatoa maji Yake.

101 Lakini ilikuwa ni kitu gani? Hebu tumwangalie mzee huyo, yeye yuna umri wa miaka mia moja na ishirini.

102 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Mungu ni Mungu asiye haki," kasema, "kwa sababu alimwaibisha Musa. Baada ya yeye kuteseka na hao Waebrania kwa muda wa miaka arobaini kwenye hilo jangwa huko nje, Yeye alimwaibisha na hata asingemruhusu kuingia kwenye nchi ya ahadi."

103 Nikasema, "Loo, upuuzi!" La, Yeye hakumwaibisha Musa. Yeye alienda kwenye nchi ya ahadi. Yapata miaka mia saba baadaye, alionekana juu ya Mlima wa Kugeuzwa Sura, akiwa hai alivyopata kuwa, amesimama, akizungumza na Yesu kabla Yeye hajaenda Kalvari, yeye pamoja na Eliya, wamesimama pamoja, wakizungumza, pia. Musa na Eliya waliwatokea Yesu, Petro, Yakobo na Yohana, juu ya Mlima wa Kugeuzwa Sura. Hakuwa amekufa. Alikuwa hai. Mungu hakumwaibisha. Yeye alikuwa huko Palestina.

104 Sasa angalia, kabla hajafa, yeye alipanda Mlima Nebo, asubuhi ile wakati alipojua anaondoka. Aliisha mvua Haruni nguo, akamvalisha mtu mwingine nguo zake. Akachukua vazi lake mwenyewe, akaliweka juu ya Yoshua, akamwamuru kuzishika hizo amri! Ndipo wakati alipopanda juu ya Mlima Nebo, akapitia kwenye bonde la nchi tambarare, akijua alikuwa akienda huko juu apate kufa, na akapanda juu ya Mlima Nebo, na kupanda juu ya Pisga. Basi alipokuwa amesimama kule juu, Mungu alisema, "Iangalie ile nchi. Ninataka uione. Musa, ungalienda kule. Bali unajua ulichofanya huko chini kwenye Mwamba ule siku ile? Ulijitukuza mwenyewe." Nafikiri hiyo ndiyo itakayokuwa shida kubwa kwetu watu wengi leo. "Ulienda kule chini kwenye Mwamba, nawe ukajitukuza." Lakini angalieni wakati alipokuwa tayari kufa, ule pale ule Mwamba ulisimama. Hapana budi aliukanyaga tu Mwamba huo pale Pisga, kisha Mungu akamzika. Lakini hapana shaka alifufuka tena, mahali fulani, kwa kuwa yeye alikuwa hai. Yeye

alikuwa ni mfano wa Kristo. Huyo hapo, amesimama juu ya Mlima wa Kugeuzwa Sura, mamia ya miaka baadaye, huko Palestina. Mnaona, neema ya Mungu iliutoa Mwamba. Loo, jamani!

105 Ninapowazia juu ya Ibrahimu, juu ya makosa yote aliyofanya, na Musa na kosa lake, lakini wakati wasifu wa Ibrahimu ulipoandikwa, wakati wasifu wa Kiungu ulipoandikwa, wakati Paulo alipouandika wasifu wa Ibrahimu, kamwe hakutaja neno moja kuhusu kutokuamini kwa Ibrahimu. La, la, hata haikuhesabiwa kwake kamwe. Yeye alisema, "Ibrahimu hakusita kwa ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimpa Mungu sifa."

106 Ombi langu nyenyekevu ni, mbele za neema ya Mungu iliyo hapa asubuhi ya leo, ninatumaini yangu itaandikwa jinsi hiyo, ya kwamba Yeye hatayaona makosa yangu. Ya kwamba wakati wasifu wangu utakapoandikwa, rambirambi zangu, ya kwamba hazitasema ya kwamba nilifanya makosa na kutenda mabaya, bali Yeye ataona tu mambo niliyojaribu kumfanyia. Naomba yawe tu...Ni kitu gani kinachofanya hilo? Yeye ataichukua neema ya Mungu ninayoiamini. Na hapo ndipo ninapotumainia pekee. Kwa kuwa juu ya ustahilifu wangu mwenyewe nisingeweza kuingia kuliko yeyote yule wa hao wengine, bali ninaitegemea neema ya Mungu. Naam, ni neema ndiyo ninayoitegemea.

107 Kulikuwako na Mwamba pale wakati Musa alipokuwa tayari kufa.

108 Tungeweza kusema nini juu ya Daudi? Neema ya Mungu! Yule askari mkuu wa vita ambaye Mungu Mwenyewe... Yeye alisema, "Yeye ni mtu anayeupendeza Moyo Wangu Mwenyewe." Huyo askari mkuu wa vita, Daudi, angewezaje kufanya kitu kama hicho alichofanya, kumchukua Uria, askari wake, wakati alikuwa na Wamataifa kadha huko nje kama askari? Sikilizeni kwa makini hadithi hii ndogo kwa dakika moja. Wakati walikuwa na askari wao huko nje, na Uria alikuwa ndiye aliyesimama na Daudi. Uria alikuwa mwongofu, alikuwa ni Mhiti, mwongofu wa dini ya Kiyahudi. Nao hao watu walimpenda Daudi sana! Waliona upako ulikuwa juu yake, ingawa alikuwa ninii—alikuwa ni mtoro. Alikuwa amefukuzwa nchini mwake mwenyewe, akalazimika kuishi na Wafilisti. Sauli alikuwa akimwinda. Lakini hata hivyo watu hao, waliuona upako juu yake! Walijua alikuwa akija mamlakani. Utukufu kwa Mungu!

109 Nina furaha sana kuwa mtoro leo, kwa sababu ninaona ya kwamba Kristo anakuja kuwa Mfalme. Mnaweza kuwachagua akina Kennedy wote na wowote wale mnaotaka. Lakini Kristo atakuwa Mfalme! Upako uko juu Yake, juu ya Ujumbe Wake wa Kuja Kwake. Naye atakuwa Mfalme!

110 Wao walifanya nini? Siku moja alikuwa amesimama pale ana kiu ya maji ya kutoka langoni huko Bethlehemu, mahali alipokuwa akienda kuwachunga kondoo. Nanyi mwajua nini? Wawili wa hao watu wakachukua panga na kufyeka kupitia maili kumi na tano za miili ya binadamu, wapate kumchotea ndoo ya maji. Kwa maana, mbona, shauku yake iliyo ndogo sana ilikuwa ni amri kwao. Wazia jambo hilo! Nao wakafyeka kupitia kwa watu hao, kote kote mpaka juu ya ule mlima mahali ambapo walisema alikuwa amesimama, ingekuwa ni karibu maili kumi na tano. Walipitia pale. Na kila mtu aliyesimama, wangepigana naye kwa mapanga mpaka wamwue. Wakapitia pale! Nao wakachukua hii ndoo na kuchota ndoo ya maji, moja kwa moja kupitia kwa ngome ya adui, watu wawili, kumchotea mfalme wao, ndugu yao, maji ya kunywa. Ingawa, yeye alikuwa na maji kule juu ya kunywa, bali alitaka *yale* maji.

111 Ee Mungu, jalia niuchukue Upanga wa Neno na kufyeka kupitia kwa kila shirika, kuuleta ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, na Nguvu za ufufuo na Roho Mtakatifu, zirudi kwa watu, pasipo kujali ninii . . . kwa kuwa Yeye yuaja mamlakani. Yeye anakuja mamlakani, atasimama peke yake. Bali ni kufyeka kupitia kwa kila dhehebu, kufyeka kupitia kwa kila nadharia, kila kanuni za imani za kujibunia, mpaka utakapomrudishia Mwokozi kondoo aliyepotea, mtu fulani, kuyarudisha Mafundisho ya Biblia tena, ya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Neema ya Mungu!

112 Mwangalie Daudi. Yeye angaliwezaje kufanya . . . Yule aliyeruka shimoni na kumwua simba. Daudi angewezaje kumchukua mke wa Uria, Bethsheba mrembo, wakati alipokuwa na mia tano wake mwenyewe? Lakini alimwona akioga. Na huo hapo uzembe. Sasa, yeye alisahau tu kuvuta pazia wakati alipokuwa akioga, naye alijua mfalme alikuwa akitembelea pale, karibu na pale, kila siku, huko chini juu ya ule ukuta.

113 Hiyo ndiyo shida. Sidhani siku hizi wanawake wanazembea hivyo ama chochote kile, vema, wao kwa urahisi wanatoka tu wanaenda uchi, hivyo tu, mitaani, wamevalia maskini nguo fupi. Ni fedheha! Halafu mnashangaa ni kwa nini wanaume wanapiga mbinja na mluzi. Mbona, wao wanafanya hivyo kuwafanya wapige mbinja na kufanya yasiyofaa. Wanajua hilo, wana akili za kutosha kujua hilo. Wanafanya hivyo kwa sababu tu wanataka kufanya hivyo. Liko moyoni mwao. Ukiwaambia ya kwamba wao ni watovu wa uadilifu, huenda wakabishia hilo. Lakini huenda wasiwe wazinzi, huenda wakawa ni safi sana kama yungiyungi, ikifikia kujuana kimwili. Lakini, kumbukeni, kuna pepo juu yao, ule upako wa ibilisi, ukiipeleka nafsi ya mwanamume fulani kuzimu. Kumbukeni, Biblia ilisema, "Kila amtazamaye mwanamke, kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Pia kumbuka, dada, utawajibika kwa kufanya uzinzi ingawa

kweli hukuufanya maishani mwako mwote, lakini yule mwenye dhambi aliyekuangalia jinsi ulivyovalia, yuna hatia ya uzinzi. Utawajibika kwenye Siku ya Hukumu, kwa kufanya uzinzi. Wakati inapomlazimu kusema . . .

114 Yeye anasema hapa, ameandika kwenye Kitabu Chake, "Kufanya uzinzi."

"Na nani?"

"Bibi John Doe."

"Basi, Bibi John Doe, na hilo je?"

115 "Naapa mimi . . . Unajua kumbukumbu yangu, kamwe sijapata kuishi na mwanamume mwingine ila mume wangu."

116 "Lakini ulijivalisha nguo mpaka ukamfanya huyu mtu kufanya uzinzi. Nawe una hatia ya uzinzi pamoja naye. Hapo ndipo alipoufanya. Wewe una hatia, wewe ndiwe uliyejianika."

117 Bathsheba alifanya kosa kama vile Hawa alivyofanya kosa, lakini Adamu alihesabiwa katika hilo. Nafikiri sikuzote tunapiga makelele kuhusu wanawake, pia. Ninyi wana wa Mungu, wanaume. Ninajua ninyi ndinyi kundi lililo na nguvu kuliko wote, hiyo ni kweli, jinsia iliyo na nguvu zaidi. Mko juu ya wanawake, hiyo ni kweli, kwa hiyo fanyeni kama hivyo. Msiwashinde nguvu, kujaribu kumchukua msichana mdogo na kuyaangamiza maisha yake. Lakini kuwa mwana wa Mungu, mwambie amekosea, na usimame kama mwana wa Mungu. Yeye ni dada yako. Naam, bwana. Tunachojaribu kufanya, wale wanaoitwa wana wa Mungu leo hii, ni wafuasi wa makanisa, humchukua kila msichana mdogo wawezaye. Kumbukeni, sababu ya kuwako na mwanamke mchafu huenda ikawa ni kwa sababu mwanamume fulani aliyeoa aliyaangamiza maisha yake, pia. Kwa hiyo, chungu hakiwezi kuiita birika kwamba ni nyeusi, kwa hiyo kumbukeni tu. Dhambi ndiyo inayofanya hayo yote. Nasi sote tunapasiwa mauti, na tunapaswa kufa kwa ajili yake.

118 Wakati Daudi alipofanya jambo hilo ovu, hukumu yake mwenyewe ilipaswa kumwua. Wakati yule nabii alipokuja kule juu, alidhani lilikuwa limefichika. Wakati yule nabii alipokuja kule juu na kusimama mbele zake, yeye alisema, "Daudi, kila kitu kinaendelea vizuri?"

Kasema, "Kila kitu ni sawa."

119 Daudi, katika mavazi yake ya kifahari na taji yake kubwa, naye alikuwa amemtuma Yoabu huko nje, jemadari wake mkuu, na vita vyote vikiendelea. Alikuwa akiwasukuma maadui wote nje ya mipaka yao na kadhalika, kila kitu kilikuwa kikiendelea vizuri. Alipata mtoto kwa huyu Bathsheba. Naye alimfanya maskini Uria kwenda huko nje, kisha akamfanya Yoabu asimame karibu naye, mpaka alipomwondokea. Na—na—na mvulana huyo akafa wakati jua lilipotua, akiwa na kisu cha vita mkononi mwake, damu kwenye ngao yake, ambapo alikuwa

amewapigania Israeli, ingawa alikuwa ni mwongofu kwa dini yao. Ndipo wakati Yoabu aliporudi na kumwambia ya kwamba—ya kwamba Daudi alikuwa amekufa . . . ya kwamba—ya kwamba Uria alikufa, Daudi aliwazia, "Kila kitu ni shwari sasa. Nimempata mke wake, na kila kitu kitakuwa ni sawa. Amemzaa mtoto." Lakini mtoto huyo akashikwa na ugonjwa. Mtoto huyo akaanza kufa. Naye akafanya kila alichoweza kuyaokoa maisha ya mtoto huyo, labda kila daktari alikuja. Haikufaa kitu. Hatimaye, mtoto huyo akafa. Waliogopa kumwambia Daudi kwamba mtoto alikuwa amekufa. Naye akafa. Ndipo akafikiri kila kitu kilikuwa kimefichwa. Kwa hiyo akamfariji Bathsheba. Alikuwa tayari amemchukua kama mke wake, baada ya hao wake wengine wote.

120 Huyu nabii mkongwe, maskini jamaa mwenye upara akaingia kwa kishindo, mzee Nathani, kutoka nyikani, akaketi, kasema, "Daudi, mambo vipi?"

121 Kasema, "Sawa! Sawa! Nabii mzee wa Mungu, ishi milele! Haleluya!" Loo, alikuwa ninii tu . . . Alidhani kila kitu kilikuwa ni shwari, alidhani angeweza kulificha.

122 Lakini huwezi kujificha kutoka kwa Mungu! Anajua unachowazia sasa hivi. Anayajua mawazo yako, kwa kuwa Yeye ni Mungu. Huyo Roho Mtakatifu aliye humu jengoni asubuhi ya leo, anayajua mawazo yako, kwamba wewe ni nani, mahali unapotoka, yale umefanya, kwa kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana leo, na hata milele.

123 Mungu alikuwa amemfunulia huyo nabii. Akasema, "Daudi, kulikuwako na tajiri aliyeishi upande *huu* wa barabara, alikuwa na kondoo wengi sana, loo, alikuwa tajiri sana. Mtu mmoja aliishi upande *huu* wa barabara, alikuwa maskini, alikuwa na mwana-kondoo mmoja. Alimchukua kama binti yake. Alimlisha kwa kijiko kile kile alicholia. Alilala pamoja na mwana-kondoo huyo. Kila kitu kilikuwa ninii tu . . . Alikuwa tu ni kama binti kwake. Basi siku moja mgeni akaja, kwa hiyo, badala ya tajiri huyo kumchukua mmoja wa kondoo wake mwenyewe na kumwandalia karamu mgeni wake, vema, badala yake, alienda kule na kumchukua mwana-kondoo wa yule maskini, na kwa kutumia nguvu, akamchukua mwana-kondoo huyo na kumchinja, na kufanya karamu."

124 Sasa, hiyo ilikuwa ni tamaa kali ya Daudi. Alikuwa na wake mia tano, lakini wakati alipomwona mke wa Uria, badala ya kuchukua mmoja wa wake zake mia tano, kutuliza ama kuridhisha tamaa yake, alienda, akamchukua mke wa mtu huyu mwingine, kisha akamwua Uria wakati mke aliposhika mimba. Daudi hakujua kile alichokuwa akifanya, mbona, Daudi alikuwa tayari kutoa hukumu. Hivyo ndivyo tulivyo sisi. Daima tunaweza kumhukumu jamaa huyo mwingine, lakini inapotufikia sisi, loo, hilo ni tofauti.

125 Daudi alisema, “Mtu huyo atalipa kwa uhai wake.”

126 Nabii huyo mzee, hayo macho yakafinya. Akasema, “Daudi, hakika hutakufa!” Angalia neema hapo ikiingia kazini upesi sana. Roho alimchochea nabii, akayaokoa maisha ya Daudi. Neema, “Hakika hutakufa, bali upanga hautaondoka nyumbani mwako mpaka utakapoutakasa moyo wako kabisa. Kwa kuwa, wewe ndiye huyo tajiri.” Loo, ilikuwa ni tofauti wakati huo, sivyo?

127 Ni kitu gani kilichomwokoa Daudi, wakati hukumu yake mwenyewe ilisema, “Mtu huyo atakufa! Yeye ataijutia kwelikweli, naye atailipia kwa uhai wake”?

128 Ndipo nabii akasema, “Hakika (neema) hutakufa. Hutakufa, Daudi. Neema imekuokoa.” Ilikuwa ni neema, kwa Daudi, iliyomwokoa. Loo, jamani!

129 Kama isingekuwa ni neema, sote tungekuwa wapi? Hiyo ni kweli? Hakika.

130 Neema kuu inatoka kwa Aliye mkuu. Neema kuu kutoka kwa Aliye mkuu. Ukuu, unaweza kufanya nini? Ukuu unaweza kufanya chochote utakacho. Sikilizeni hili sasa. Neema kuu inaweza tu kutolewa na Yule Aliye Mkuu. Naye Mungu ni Mkuu, kwa hiyo anaweza kutoa neema kuu. Kwa hiyo kwa kuwa ni Kuu, neema si lazima imuulize mtu yeyote, si lazima. Hufanya kile itakacho. Si ni ajabu hiyo? Si lazima iulize, “Naweza kufanya *hili*? Ama, nifanye *hili*? Je! naweza? Inanibidi kulifanya? Nitafanya?” Haifanyi hivyo. Inafanya hivyo yenyewe. Neema ni Kuu, kwa hiyo Yeye anaweza kumwokoa aliye mbaya kuliko wote, anaweza kumwokoa aliye mwovu kuliko wote, anaweza kumwokoa aliye mchafu kuliko wote, anaweza kumwokoa mtovu wa maadili kuliko wote, anaweza kumponya aliye mgonjwa kuliko wote. Haleluya!

131 Anaweza kumwokoa aliye mwovu kama mimi. Naye aliniokoa. Ni kitu gani? Neema! William Branham, mwana wa mlevi. Hilo halileti tofauti yoyote, neema ya Mungu iliniokoa!

132 “Mimi, mimi ni binti ya mwanamke ambaye hakuwa mzuri.” Haileti tofauti yoyote, neema ya Mungu ilikuokoa. Ni Kuu, haiibidi kumwuliza mtu yeyote chochote. Amina! Nina furaha sana kwa hilo. Haleluya!

133 Inaweza kumchukua mwenye dhambi aliye mwovu kuliko wote na kumfanya mweupe kama theluji, haihitaji kumwuliza mtu yeyote juu yake. Loo, inaweza kufanya hivyo kwa sababu ni Kuu. Sikilizeni, upesi sasa.

134 Hiyo ilithibitishwa pale msalabani, wakati palipokuwapo na mwizi aliye mwovu kuliko wote, alistahili kufa. Kamwe hakuwa amemwazia Mungu moyoni mwake. Kamwe hakuwazia lolote juu Yake. Pale msalabani wakati, kupitia kwa hiyo

midomo iliyojaa damu, kati ya kuugua kulitokea sauti, "Bwana, unirehemu!"

135 Ndipo ikatokea nyingine kupitia kwa Damu, machozi, maumivu makali, neema ilitia nanga na kusema, "Leo hii utakuwa pamoja Nami Paradiso." Neema ilifanya jambo hilo. Huyo mwizi angejisaidiaje? Si zaidi ya vile Adamu angalijisaidia, si zaidi ya vile Hawa angalijisaidia, si zaidi ya vile ungeweza kujisaidia, si zaidi ya vile ningeweza kujisaidia, si zaidi ya vile tungaliweza kujirusha huko juu kwenye Kilimia Angani kwa nyugwe za mabuti yetu. Tusingeweza kufanya hivyo. Lakini neema ya Mungu inaweza kufanya jambo fulani kulihusu, nayo hufanya! Neema ya Mungu, ukuu wa neema ya Mungu, ulimjia yule mwizi aliyekuwa akifa, "Leo hii utakuwa pamoja Nami Paradiso." Loo, wazia hilo! Ajabu hiyo.

136 Wazieni juu yake: Upendo na neema ni dada, dada mapacha. Huwezi kuwa na neema pasipokuwa na upendo. Hao ni dada mapacha. Kweli kabisa. Kabla hujaweza kupata neema, huna budi kuwa na upendo. Kabla kweli hujamwonyesha mtu fadhili, unawapenda; sahihi ama makosani, huna budi kuwapenda, kwa vyovyote vile, la sivyo huwezi. Unaona? Kwa hiyo upendo na neema ni kitu kile kile. Hao ni dada mapacha tu, hivyo tu, upendo na neema. Wao, sisi tulikuwa. . .Hatuwezi kumwona mmoja bila huyo mwingine. "Mungu aliupenda ulimwengu, akamtoa Mwanawe pekee," Yeye alitoa neema Yake, na kuileta mioyoni mwetu kupitia Roho Mtakatifu. Mnaona? Hakuna kabisa kitu unachoweza kufanya bila ya kutenda kazi na moja kwa nyingine. Neema, neema ya Mungu ndiyo inayotuokoa.

137 Sasa tunaona, hiyo neema, hapo kama huyo mwizi aliyekuwa akifa, si ajabu imewavuvia washairi walipoiona. Mshairi mmoja alisema:

> Yule mwizi wa kufa alifurahia kuiona
> Ile chemchemi katika siku zake;
> Hapo nijalie, ingawa ni mwovu kama yeye,
> Nizioshe dhambi zangu zote.
>
> Tangu hapo kwa imani nilipokiona kile kijito
> Kilichotoka kwenye majeraha Yako,
> Upendo wa ukombozi umekuwa wimbo wangu,
> Nao utakuwa mpaka nitakapokufa.
>
> Ndipo katika wimbo bora, mtamu,
> Nitaziimbia nguvu Zako za kuokoa,
> Hapo maskini ulimi huu unaopiga kitembe na kugugumiza
> Utakaponyamaa kaburini.

Neema, neema ya ajabu! Haleluya! Mmoja aliiandika:

Ee, upendo wa Mungu, ni mwingi na safi jinsi
gani!
Jinsi usivyopimika na una nguvu!
Utadumu milele,
Wimbo wa watakatifu na malaika.

Kama tungaliijaza bahari kwa wino,
Na kama mbingu zingaliumbwa kwa karatasi
ya ngozi;
Na kila shina duniani liwe ni kalamu,
Na kila mtu kazi yake ni uandishi;

Kuandika upendo wa Mungu aliye juu
Kungeikausha bahari;
Wala gombo hilo halingeweza kuuenea wote,
Hata lingalitandazwa mbingu kwa mbingu.

138 Hivyo ndivyo ilivyo, neema, neema ya Mungu. Neema ya Mungu imeleta kivuli . . . Mungu aliileta neema maishani mwetu kwa upendo Wake kwetu. Hili hapa jambo lingine neema isiloweza kufanya; neema haiwezi kununuliwa, neema haiwezi kuuzwa. Ni neema! Inatoka kwa Aliye mkuu. Naam, bwana. Huwezi kufanya maafikiano kwa ajili yake. Unaweza kusema, "Mungu, nitafanya *hivi na hivi* kama Wewe utafanya *hivi na hivi*." Huwezi kufanya hivyo. Mungu hatafanya hivyo. Huwezi kuvuta chochote kutoka kwa Mungu. Mungu hukupa kwa neema Yake. Loo, loo, loo, jamani!

139 "Si yule atakaye wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu anayerehemu." Hiyo ni kweli.

140 Watu hulala kifudifudi. Na watu wengine walinijia . . . Ninaamini nimemwona mmoja wa hao wavulana humu jengoni leo. Mvulana wa Kimethodisti aliingia tu, na kumpokea Roho Mtakatifu, kutoka juu huko . . . Na hao wavulana wakanijia, wakasema, "Sasa, Ndugu Branham, kwa kuwa sasa tumeokoka na kumpokea Roho Mtakatifu, twende kuzitafuta karama?"

Nikasema, "Msifanye hivyo. Msifanye hivyo."

141 Mungu hutoa karama Zake kwa ukuu. Karama na miito havina majuto. Muda si muda wajua, ukianza kutafuta kitu, "Mungu, naomba unifanye tu mhubiri, nifanyie tu jambo *hili*," basi utakuwa kitu gani? Mtu mkubwa mwenye maringo, hivyo tu. Utaenda kwenye theolojia ya mtu fulani na dhehebu fulani, na huko utajisindilia chini na kuoza. Acha Mungu atoe wito huo. Mungu atakuita, Mungu atakutakasa, Mungu atakupa kile anachotaka kukupa. Naam, bwana.

142 Huwezi kufanya maafikiano kwa ajili ya neema. La, bwana. Wewe, haiwezi kuuzwa, wala haiwezi kupigiwa bei, wala haiwezi kununuliwa, haiwezi kuuzwa. Huwezi kusema, "Vema, sasa, Bwana, nitaenda nikajiunge na kanisa hili kubwa la Baptisti, ama kanisa hili kubwa la Methodisti, ama kanisa hili kubwa la

Kipentekoste, ama kanisa hili kubwa la Kinazarayo. Nitafanya *hili* kama utanifanyia tu *hili*." Haipigiwi bei. La, bwana.

143 "Wote alionipa Baba watanijia Mimi. Hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa Baba Yangu amwite kwanza."

144 Unakuwa tu mfuasi wa kanisa hilo kubwa, hivyo tu, hutaokolewa. Neema haina budi kukuokoa. Vipaji vyetu havitegemei, na vipaji vyetu haviwezi kuwa ninii ye—yetu... Vipaji vyetu tulivyo navyo, hatuwezi kupata neema kwa vipaji.

145 Kama Mungu alinifanya mhubiri, hiyo haionyeshi neema Yake imekuwa pamoja nami. La, la. Ni neema Yake pekee ndiyo iliyoniokoa. Si kwa sababu ninaihubiri Injili, ndiyo nimeokolewa. Si kwa sababu unanena kwa lugha, ndiyo umeokolewa. Loo, la. Si kwa sababu wewe, kwa sababu unahubiri. Hata huokolewi ati kwa sababu tu unahubiri. Hu—huokolewi ati kwa sababu unanena kwa lugha. Huokolewi ati kwa sababu unafanya lolote la mambo haya. Wakorintho wa Kwanza 13 inathibitisha hilo, "Nijaponena kwa lugha ya wanadamu na Malaika, nijapofahamu siri zote za Mungu (mhubiri), nijapofanya yote *haya*, na nina imani ya kuihamisha milima, si kitu mimi mpaka upendo utakapoingia, ambao ni upendo." Upendo ni neema. Neema ya Mungu inayofanya yote.

146 Watu wengine, mna vipaji kama baadhi ya hawa wafalme wa roki. Hilo linanichefua tu kwenye, sijui mimi, matumbo yangu ya kiroho. Nitawaambia, ninapowasikia hawa roki wakisimama Jumamosi usiku na kuimba roki, na kucheza dansi usiku kucha, na halafu kesho yake asubuhi wanakuja mbele ya wasikilizaji na vitu kama hivyo wakijaribu kuonyesha uso mrefu wa kuiga utakatifu, na kusimama pale juu mbele za watu na kuimba wimbo wa kanisa, na kuwazia wanaenda Mbinguni. Ningeweza kuyataja majina mengi, bali si lazima. Kanda hii inaenda kila mahali. Lakini nyote mnajua. Mvulana mmoja hapa sio muda mrefu uliopita, huko Hollywood, asingembusu msichana kwa sababu ilikuwa ni kinyume na "dini" yake. Kinyume na "dini" yake, na kufanya picha za roki na kadhalika ambazo ni za aibu sana, na vitu kama—kama hivyo. Unafikiri ya kwamba ungechukua vipande vyako thelathini vya fedha na kustahili kitu fulani katika neema ya Mungu, ewe Yudasi? Havitakununulia kitu ila mahali fulani katika kuzimu!

147 Neema ya Mungu haiwezi kupigiwa bei, wala kuninii... kupatikana kwa vipaji. Ni neema kuu! "Sina cha mkononi ninacholeta, naushikilia tu msalaba Wako." Uchi, nimejeruhiwa, ninakuja tu jinsi nilivyo.

> Hivi nilivyo, bila hoja moja,
> Ila kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa ajili
> yangu,
> Na kwamba Wewe waniita nije Kwako,
> Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja!

148 Hivyo tu, neema ndiyo iliyonileta. Neema ilifanya hivyo. Neema ni kama, jambo lingine ningetaka kusema, wakati mwingine neema ni . . .

149 Makanisa haya makubwa, wanafikiri ya kwamba unaweza kushuka uende kule, wanawazia, "Vema, tulijenga kanisa lililo kubwa kuliko yote mjini. Tuna shirika la misaada la wanawake hapa linalowafanya maskini. . .nguo kwa ajili ya maskini, na kuzituma katika nchi za ng'ambo. Tunawalisha maskini. Tunafanya yote *haya*."

Paulo alisema, "Ninaweza kufanya jambo lile lile, na si kitu."

150 Wao wanasema, "Vema, sisi, sisi ni shirika la kale. Tumekuwa hapa kwa muda wa miaka elfu mbili. Tuna umri wa miaka mia tano. John Wesley, Alexander Campbell, na hao waanzilishi mashuhuri huko nyuma, walilianzisha kanisa letu. Haleluya!"

151 Vema, Yesu Kristo alilianzisha Kanisa hili, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuwaambia wapande waende kule Pentekoste na wangojee mpaka walipozipokea Nguvu kutoka Juu.

152 Na bado unaweza kuwa mfuasi wa kanisa la Kipentekoste na upotee. Kanisa la Kipentekoste si zaidi ya kanisa lingine lolote. Hiyo ni kweli.

153 Jambo ni kwamba, kuna Kanisa moja tu, hilo ni Kanisa unalozaliwa ndani yake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, "Kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," Wakorintho wa Kwanza 12:13, hiyo ni kweli, Wakorintho wa Kwa—Kwanza 12. Sasa, tunabatizwa katika Kanisa hilo.

154 Lakini watu wanafikri ya kwamba wanaweza kujistahilisha. "Mbona, sisi, ni—nilienda shuleni na nikajifunza kufanya *hili*, na nilienda kwenye seminari na nikafanya . . . " Hilo halimaanishi jambo moja. Huwezi kuinunua neema ya Mungu.

155 Neema ya Mungu iko hivi. Hebu niwasimulie hadithi moja, katika kumalizia. Neema ya Mungu iko hivi. Wakati mmoja kulikuwako na mfalme mwenye nguvu, naye mfalme huyu mwenye nguvu alikuwa na mwana naye alikuwa ni mwanawe wa pekee. Basi siku moja mwuaji alimwua mvulana huyo. Ndipo kote katika ufalme huo wakaenda wajumbe wakimtafuta huyo mwuaji. Hatimaye walimpata huyo mwuaji. Ndipo walipompata, walimrudisha na kumfunga gerezani. Basi walipofanya hivyo, kesi ilifanywa na uamuzi ukatolewa. Loo, lilikuwa ni jambo baya sana. Alikuwa amemwua kinyama mwana wa mfalme, naye alijua lililokuwa linamjia.

156 Wakamweka katika seli za ndani, wakaifunga milango, wakaifunga kwa kufuli kusudi mtu yeyote. . .walinzi wamelizunguka, maana tunajua ni adhabu mbaya jinsi gani kijana huyu atakayoipata, kwa sababu yeye alimwua mwana

wa mfalme, wa kifalme, mwana wa mfalme. Walinzi waliwekwa kote kuizunguka milango. Aliwekwa kwenye seli za ndani. Akavuliwa nguo, akabaki tupu ila ki—kipande cha nguo cha kiuoni. Naye huyo hapo, ameketi pale katika hali hiyo. Akifa kwa njaa, wasingempa chakula. Alikuwa ameketi katika hali hiyo.

157 Ndipo wakamleta kwenye kesi. Alipatikana na hatia na kuthibitishwa kuwa na hatia. Hukumu ikatolewa, kwamba atauawa chini ya adhabu kali sana ya kifo, angeuawa polepole mpaka uhai wake wa kibinadamu utakapotoka. Akahukumiwa na hakimu, alikuwa afe. Naye akasihi na kulia, naye akasema, "Ingawa nina hatia, ingawa nina hatia, ninasikitika kwamba nilifanya hivyo. Laiti nisingalifanya hivyo. Nasikitika kwamba nilifanya hivyo. Katika dakika moja, kwa hasira kali, nilifanya hivyo. Sikutaka kufanya hivyo."

158 Siku moja mfalme huyo alishuka akaenda mahali pale, kumtembelea mvulana huyo, kumwambia, kuzungumza naye na kumwambia juu ya kumwua mwanawe, mwana wa pekee aliyekuwa naye. Yeye alikuwa amemwua mvulana huyo. Akasema, "Ninaenda kuzungumza naye."

159 Basi aliposhuka kule, aliangalia nyuma kwenye hicho kizimba, kama mnyama aliyewekwa kwenye kizimba. Aliona maskini mwili wake uliokonda sana umelala kule nyuma pembeni, akilia. Uso wake ulikuwa umezama ndani, mashavu yake yamezama nyuma, macho yake huko nyuma kabisa, matongo yalikuwa yamejaa machoni mwake, na kinywa chake chote kimekuwa cheupe; hamna maji, ana kiu. Amelala huko nyuma kifudifudi, analia. Mfalme akasema, "Simama." Akamjia, naye akamwangalia. Akasema, "Kwa nini ukamwua mwanangu? Kwani mwanangu alikufanya nini? Alifanya nini kustahili kifo kama hicho ulichomwua, ukamchoma mkuki akafa?"

160 Akasema, "Hakuna, bwana wangu, hata kitu kimoja. Ni ujeuri wangu tu, njia zangu tu. Nilimwua kwa sababu nilimwonea wivu, nami nikashikwa na hamaki na nikamwua." Kasema, "Sasa mimi nitakufa chini ya haki yako, bwana. Ninatambua jambo hilo na ninastahili kufa. Jambo pekee ninalolilia, ni kwamba ninasikitika nilimwua mtu huyo wa kifalme namna hiyo, bila sababu."

161 Mfalme akaharakisha akatoka nje, akaenda kwenye dawati, na akasema, "Angamizeni kumbukumbu zote!" Mwajua, ziwekeni kwenye bahari ya usahaulifu. "Angamizeni kumbukumbu zote! Mwosheni, msafisheni. Nitatuma vazi kwa ajili yake."

162 Baada ya kitambo kidogo, limosini kubwa mno ikaja mlangoni. Ilipokuja, zulia lilitandikwa chini hata kwenye seli ya gereza. Mfalme akasimama mwishoni mwa limosini

hiyo, kasema, "Njoo, mwanangu, upande gari uende nyumbani pamoja nami kwenye ikulu," akaweka vazi la mfalme begani mwake. Akasema, "Tangu sasa na kuendelea wewe ni mwanangu."

163 Kwa sababu alikuwa na huruma, hiyo ni neema. Huyo alikuwa ni mimi, huyo alikuwa ni wewe. Tulimwua Mwana wa Mungu, kwa dhambi zetu. Tulikuwa wageni, wachafu, wenye kinyaa, tumewekwa kwenye seli za ulimwengu. Mungu alituosha kwa Damu ya Mwanawe Mwenyewe, na kutusafisha, akatuvisha vazi la Roho Mtakatifu. Na sasa lile gari kuu la Mungu litasongezwa mlangoni siku moja, nasi tutaenda nyumbani tukaishi pamoja na Yeye. Kumbukumbu zote zimeangamizwa, hatuwezi kuhukumiwa tena; zimeteketezwa kwa moto, Yeye akaziweka katika bahari ya msamaha wala hazikumbuki tena. Si ajabu tunaweza kuimba!

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika ni tamu,
Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
Na nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
Neema ikaniondolea hofu zangu;
Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
Ile saa niliyoamini!

164 Hivi hutaacha hii iwe ndiyo saa yako hivi sasa, rafiki mwenye dhambi, wakati tukiviinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi mafupi? Hebu hii na iwe ni saa uliyoamini kwa mara ya kwanza, sasa hivi. Amua, na useme, "Bwana Mungu, mimi nina hatia. Ninatambua inahitaji neema kuniokoa mimi. Siwezi kujiokoa. Nimepotea. Nimekwisha. Kamwe siwezi kufanya lolote. Si—si—sijiwezi kabisa, bila matumaini, bila Mungu, bila rehema, bila Kristo, ulimwenguni, nimetengwa. Hivi hutakuwa na rehema na kunitoa kwenye seli hii ya dhambi niliyomo leo hii, Ee Bwana? Na unirehemu, nili mwenye dhambi." Waweza kuinua mkono wako, useme, "Bwana Mungu, mimi ni mtu huyo anayehitaji neema Yako"? Waweza kuinua mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham, sasa nitaamini"? Mungu akubariki huko nyuma, ndugu yangu.

165 Mtu mwingine aseme, "Ndugu Branham, nikumbuke sasa, loo, ndugu, naomba unikumbuke, katika maombi." Mungu akubariki, mama. "Omba ya kwamba . . . " Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, ndugu, hapa kwenye dirisha. Mungu akubariki, ndugu, huko nyuma. Mungu akubariki, ndugu, upande huu, huyo mwingine. "Nikumbuke, Ndugu Branham." Mungu ambariki ndugu yangu pale. Naam, huyo mwingine hapa. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki

hapa, ndugu. Yeye anakuona sasa. Limaanishe kabisa. Mungu akubariki, kijana. Yeye huona, anajua. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada anayeegemea ukutani. Mungu akubariki hapa chini, ndugu. Mungu akubariki, ndugu huko nyuma unayeegemea ukutani.

> Hivi nilivyo, bila . . .

Kungekuwako na mwingine? Mungu akubariki. Ninauona mkono wako huko nyuma.

> Ila kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa ajili yangu,

Naam, Bwana. Mungu akubariki, dada.

> Na kwamba . . . (Mungu akubariki, dada.) . . . Wewe waniita nije . . . (Mungu akubariki, huko nyuma . . . ? . . .) . . . Kwako,
> Neema, neema, Na- . . . (Mungu akubariki, ewe msichana) . . . naja!

> Hivi nilivyo, na bila kungojea
> Kuiondolea nafsi yangu doa moja jeusi,
> Kwako, Wewe ambaye Damu Yake inaweza kusafisha kila waa,
> Ee Mwana-Kondoo wa . . . (neema, loo, neema) naja! Naja!

166 Sasa, kumekuwako na yapata mikono kumi na mitano ama ishirini iliyoinuliwa. Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nitawaulizeni ninyi mlioinua mikono yenu, kwa utulivu sasa simameni tu kwa miguu yenu wakati nikiwaombea dua. Hatuna nafasi hapa juu madhabahuni. Ni niniii tu, siwezi. Ninyi simameni kwa miguu yenu, kila mtu aliyeinua mkono wao, wanaotaka kuombewa sasa. Simameni kwa miguu yenu sasa hivi wakati nikiwaombea. Simameni tu kwa miguu yenu; kila mahali.

> . . . ilimwagwa kwa ajili yangu,
> Na kwamba . . .

Hilo ni sawa. Mungu akubariki . . . ? . . .

> . . . nije Kwako,
> Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja!

167 Kumbukeni, huenda kukawa na siku ambapo neema haitakaa tena, haitadumu kwenu tena, itakuwa imechelewa kupita kiasi. Sasa haijachelewa kupita kiasi.

168 Ee Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye alimfufua tena Mwokozi wetu katika wafu, sasa yu hai, Yeye aliye mkuu Utukufuni, akimtuma Roho Mtakatifu wa Kristo juu yetu, kuleta sadikisho la dhambi kwa mwenye dhambi. Mungu, ninawaombea watu hawa waliosimama kwa miguu yao. Ni kweli, Bwana. Wewe ulisema, “Yeye atakayenishuhudia Mimi

mbele ya watu, huyo nitamshuhudia mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu." Tunajua, tutakaposimama kwenye ile asubuhi kuu ya hukumu, utakuwa ni wakati wa jinsi gani. Wao wanasimama sasa, Bwana, ili dhambi zao ziwatangulie; dhambi za watu wengine huwafuata. Watu hawa wanasimama hapa asubuhi ya leo kwa sababu wanatubu dhambi zao, wakijua ya kwamba wamefanya makosa nao wanakutaka Wewe kama Mwokozi wao. Wewe huzichunguza hatamu za mioyo, na unajua yote kuwahusu.

169 Ninaomba, Baba, ya kwamba utayajalia maombi yao. Waokoe. Wao ni tunu za Ujumbe huu mdogo asubuhi ya leo, wa neema ya Mungu; haidhuru tumefanya nini, ingali inainama na kutuchukua. Tujalie, Bwana. Ijalie mioyo hii neema. Jalia wao daima wamwone Yesu kama Mwokozi wao. Wao wamefanya tendo. Roho Mtakatifu amewaambia wasimame, nao wakasimama. Roho Mtakatifu akiwaambia wasimame. Nao, kwa kumtii Roho, wakasimama.

170 Sasa, Bwana, Wewe hutimiza Neno Lako. Ulisema, "Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Yeye atakayenijia Mimi, sitamtupa nje kamwe. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala kamwe hatakuja hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Kwa hiyo, Bwana, juu ya msingi wa Maandiko haya, hayo ni Maneno Yako Mwenyewe, Bwana, ambayo tunasoma katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ambaye angeyasikia Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna!" Kwa nini? Kwa sababu ameamini, neema imemtembelea. "Amekuja kwenye Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni (ataenda mbele ya hukumu), wala hataingia hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ee Mungu, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili!

171 Tunaomba sasa ya kwamba utawaweka kote katika maisha. Wajalie, kila mmoja, abatizwe, akiliitia Jina la Bwana, ukiosha dhambi zao. Tujalie, Bwana.

172 Sasa ninawakabidhi Kwako, kama mtumishi Wako, nikiamini ya kwamba yule Malaika mkuu wa Mungu ambaye alitokea huko chini. Pia, Baba, Wewe unaijua hadithi hiyo yote, na yule Malaika mkuu aliyetokea kule Ijumaa asubuhi, mara kulipopambazuka, na kusema Maneno haya, katika umbo la pinde tatu za mvua zilizotoka juu ya mlima. Bwana Mungu, jalia huyo Mungu ambaye alinitokea kule katika pinde za mvua, jalia awaokoe hawa watu, kwa neema Yake, sasa hivi. Ninawakabidhi Kwako, katika matarajio ya Wewe kulitimiza Neno Lako, Nawe utalitimiza, nami nitakutana nao kwenye ile siku kuu, bila waa wala kunyanzi nafsini mwao. Tujalie. Katika Jina la Yesu, ninawakabidhi Kwako. Amina.

173 Mungu awabariki. Sasa wakati mkiketi chini, yeyote anayeketi karibu na hao watu ambaye ni Mkristo, peana mkono nao. Waambie, wakaribishe kanisani, na chochote kile, ili waweze . . . Loo, Yeye si ni wa ajabu?

Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika ni tamu,
Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuwa na kicho,
Nayo neema ikaniondolea hofu zangu;
Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
Ile saa niliyoamini!

Je! umeamini? Kama umeamini, inua mkono wako.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza.

Tukishakuwa huko miaka elfu kumi,
Tuking'aa sana kama jua;
Hatuna siku chache zaidi za kuimba sifa za Mungu (Mungu ashukuriwe!)
Kuliko tulipoanza mara ya kwanza.

174 Mnampenda? Sasa, Yeye si ni wa ajabu? Sasa . . .

Tukiisha . . .

Wakati tukiuimba huo tena, ninakutaka upeane mikono na mtu fulani karibu nawe, kwa utulivu sana useme, "Mungu akubariki, msafiri." Kwa utamu na utakatifu sana sasa.

Tukiisha . . . [Ndugu Branham na kusanyiko wanapeana mikono—Mh.] . . . ? . . . sifa za Mungu
Halafu tulipoanza mara ya kwanza.

Msalabani, msalabani nilipoiona ile Nuru kwanza,
Nao mzigo wa moyo wangu ukaondolewa,
Hapo ndipo kwa imani nilifunguliwa macho yangu,
Na sasa nina furaha siku nzima!

Loo, msalabani, msalabani nilipoiona ile Nuru kwanza,
Nao mzigo wa moyo wangu ukaondoka,
Hapo ndipo kwa imani nilifunguliwa macho yangu,
Na sasa nina furaha siku nzima!

Hivi hamna furaha?

Nina furaha sana Yesu huniweka huru,
Nina furaha sana Yesu aliniweka huru,
Loo, nina furaha sana Yesu aliniweka huru,
Naimba, utukufu, Haleluya, Yesu aliniweka huru,

Loo, nina furaha sana Yesu aliniweka huru,
Loo, nina furaha sana Yesu aliniweka huru,
Loo, nina furaha sana Yesu aliniweka huru,
Naimba, utukufu, Haleluya, Yesu aliniweka huru.

175 Hivi hamumpendi? Yeye si ni wa ajabu? Loo, ninafikiri tu Yeye ni wa ajabu. Sasa, wazieni tu, ya kwamba Biblia hii ni Kweli Yake, na Biblia hii inafundisha Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. . . Mungu anisamehe kwa kusema neno la kukufuru, "kama," bali ni yeye yule. Lakini kama Yeye ni yeye yule, nitaliweka hivyo, basi Yeye angekuwa ni Mtu wa aina gani? Angekuwa ni kama vile alivyokuwa.

176 Sasa, kuna tofauti moja tu katika Yeye kuwa hapa asubuhi ya leo kuliko jinsi alivyokuwa miongoni mwa watu huko Galilaya, hiyo ingekuwa ni Mwili Wake binafsi wa nyama, mwili Wake wa kawaida; kwa maana huo ulipandishwa juu (mnaamini jambo hilo?), umeketi mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, ukiishi sikuzote ili kutuombea tunapokiri. Kumbukeni, Yeye hawezi kutufanyia hata jambo moja mpaka kwanza tumkubali na kuamini ya kwamba Yeye amelitimiza, na kusema kwamba amelitimiza, kwa kuwa Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye huenda akaninii . . . Yeye ni Kuhani Mkuu anayetuombea tunapokiri.

177 Sasa wengi wenu ninyi wasomaji wa Biblia mnasema Hilo linasema "kuungama." Na *kuungama* na *kukiri* ni neno lile lile. Mnaona? "Alifanywa Kuhani Mkuu," katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 3, "sasa akituombea tunapokiri." Basi hawezi kufanya lolote mpaka kwanza tukiri ya kwamba amelifanya. Mnaona, ukishuka hapa madhabahuni na kuomba usiku kucha, halitakufaa kitu mpaka uamini ya kwamba Yeye hukusamehe, ndipo unasimama. Ndipo kadiri ulivyo na imani, hapo ndipo wewe. . . Wakati mmoja uliishi *huku* chini kabisa katika kinyaa cha dhambi. Sasa, ninyi waongofu wachanga, sasa ninyi mnaamini ya kwamba mmeokoka, sivyo? Basi mliinuliwa *hapa* juu, mkainuliwa kidogo juu zaidi. Ni kitu gani kinachofanya hilo? Imani yako, kwa sababu unaamini wewe ni Mkristo sasa, utaishi juu ya kitu hicho sasa. Unaona? Sasa kama unataka kuinuka kidogo juu zaidi, kuwa tu na imani zaidi, maana haina kikomo, inaendelea tu.

178 Vema, loo, lisilowezekana linaweza kufanywa halisi. Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Hiyo ni kweli. "Ukiuambia

mlima huu, ‘ng’oka,’ wala usitilie shaka moyoni mwako, bali uamini yale usemayo yatatimia, yatakuwa yako.”

Sasa, Yesu Kristo anaishi ndani ya watu.

179 Siku moja Kristo alikuwa katika Nguzo ya Moto, Ile unayoiona iliyopigwa picha, tunaamini kwamba Hiyo ni Yehova Mungu. Hilo ndilo Malaika yule alilokuwa akijaribu kutwambia. Sasa, Yeye alikuwa katika Ubaba wakati huo, Yeye alikuwa ni Baba wa Israeli, taifa.

180 Ndipo akaja na kuishi miongoni mwa watu Wake, kama Kristo, Mwana. Hiyo ni kweli? Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu.

181 Sasa Yeye ni Kristo, Roho Mtakatifu, ambao ni Upako. *Kristo* linamaanisha “aliyetiwa mafuta,” na Yule aliyetiwa mafuta juu ya watu, Kristo pamoja nasi, Roho Mtakatifu. Ni Kristo pamoja nasi, ndani yetu. Mnaamini hilo? Iweni na kicho sana kwa dakika moja, kwa utulivu. Sasa je! Yeye ni yeye yule?

182 Ninaamini kitambo kidogo kilichopita nilipata simu, nayo ilisema watu walikuwa wakitembea juu ya viti na kadhalika huku chini. Tutazungumzia hilo baadaye kidogo katika ibada ya kanisa. Nilimwambia Billy basi, kama walikuwa watawaombea wagonjwa, kama kulikuwa na wengi hivyo huko chini, awape kadi za maombi. Akasema angewapa. Nadhani aliwapa.

183 Kwa miezi miwili ama mitatu iliyopita, tangu wakati fulani ambapo jambo fulani lilitukia, huduma hii ilifikia mahali ambapo kidogo siwezi kuidhibiti. Wangeuona huo utambuzi na kadhalika, jinsi ambavyo ungenena na kuwaambia watu, kama tu vile hasa Bwana wetu alivyofanya alipokuwa hapa duniani. Ninyi nyote mliuona, nadhani. Ni wangapi hapa kamwe hawakuuona ama kamwe hawakuuona ukitenda kazi? Hebu tuone mikono yenu, kamwe hamjauona. Loo! Kamwe hamjauona ukitenda kazi. Vema, kuna kundi moja hapa ndani ambalo kamwe halijauona, nadhani ni wageni. Hatujui mahali watu wanakotoka.

184 Hii ni maskani ya baina ya madhehebu. Sisi hatuyapingi madhehebu, bali pia sisi—sisi hatuyaungi mkono. Tunayaacha tu yaende zao. Tunaamini katika kuwachukua watu. . .Kama wakitaka kurudi kwenye madhehebu, sawa, mradi tu wanaishi maisha ya Kikristo. Tunaninii tu—hiki hapa ni kituo tu cha kuwaokolea watu. Hivyo ndivyo huduma yangu ilivyo kwao.

185 Sasa, lakini ninaamini ya kwamba Biblia inafundisha, katika Waebrania 13:8, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.] Vema, kama ni yeye yule. . .Sasa wakati ninyi nyote mmeketi kimya kabisa kwa dakika moja, ninataka kuzungumza nanyi moja kwa moja kutoka moyoni mwangu, na kisha tutafanya ibada ya uponyaji. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, basi

Yeye alininii. . .Jinsi tu tunavyoweza kujua basi, kama Yeye ni Roho, Yeye angetenda vile vile alivyotenda jana. Hiyo ni kweli? Angetenda vile vile alivyotenda jana. Alitenda vipi jana?

186 Je! Yeye alikuwa tofauti na mtu mwingine yeyote? Yeye ni mwanadamu tu, alionekana kama mwanadamu. Alikuwa ni mwanadamu. Alizaliwa, Yeye alikuwa ni mwanadamu. Alikuwa na mwili na Damu. Aliteseka, aliugua, alipitia majaribuni. Alikuwa ni mwanadamu. Hiyo ni kweli, sivyo?

187 Lakini ni kitu gani kilichomfanya Mungu? Ni kwa sababu Roho wa Mungu alikuwa juu Yake. Yeye alikuwa ni Masihi aliyetiwa mafuta. Nao walijuaje kwamba alikuwa hivyo? Musa alisema, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii aliye kama mimi. Na itakuwa kwamba mtu asiyemsikia huyu Nabii atakatiliwa kutoka kwa watu wake." Sasa, Yeye alikuwa ni nabii. Basi je! Israeli walikuwa wakimtazamia nabii? Iliwabidi kumtazamia, kama walikuwa wakimtazamia Masihi. Naye Masihi angekuwa ni nabii.

188 Sasa hebu tuyapitie tu kwa sekunde moja, kwa sekunde chache tu, nanyi msikilize kwa makini. Sasa, iwekeni nia yenu kwa Mungu, maana hatujui yale Mungu angeweza kufanya, sijui kile atakachoniambia nifanye.

189 Ninajua ya kwamba tuna karama ya unabii kanisani. Ndugu yetu Neville, yeye huwatabiria watu, ambalo ni jambo kuu. Tunalithamini hilo. Tumekuwa tukirejea kwenye jambo hilo wakati wote. Tunao wengine hapa wanaonena kwa lugha. Hatuamini ya kwamba inawapasa watu kunena kwa lugha wapate kuwa na Roho Mtakatifu. Hakuna Maandiko kama hayo kwa jambo kama hilo. Lakini tunaamini kuna karama ya Roho Mtakatifu inayonena kwa lugha, tunayo kanisani mwetu. Lakini tunawafanya. . .Hatuendelei kupiga makelele. Tunaamini ni Sauti ya Mungu. Tunanena wakati Roho Mtakatifu anaponena, nasi tunaacha hilo lije tu mara tatu. Nalo halina budi kuninii. . .haiwezekani wakati nikihubiri ama katika utaratibu, maana roho wa manabii humtii nabii. Mnaona? Linapaswa kuendelezwa sawa kwa Biblia. Hakuna mtu anayeweza kusema ya kwamba hakuna kitu kama karama ya Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha. Tunajua hilo. Biblia inafundisha hilo, nasi tunaliamini. Na Mungu ashukuriwe tunayo kanisani mwetu hapa! Tuna karama za unabii, hizo kwanza hazina budi kujaribiwa na kuona kama ni sahihi ama si sahihi, na halafu karama ya unabii.

190 Halafu kuna nabii. Sasa, hiyo, sasa unakuja kwenye ofisi.

191 Hizo ni karama, hizo ni, kunena kwa lugha, na kufasiri lugha, na maarifa, na hekima, na utambuzi, na kadhalika. Hizo zote ni karama.

192 Lakini basi kuna ofisi tano. Ya kwanza ni mitume, manabii, waalimu, wainjilisti, na wachungaji. Hizo ni

ofisi zilizochaguliwa za Mungu. Wanadamu wanazishika, mnaona. Hizo si ninii, haziwezi . . . Huwezi kuzitamani, huwezi kuziombea; hizo zinatolewa kwa hiari kuu, unazaliwa.

193 Nabii si nabii kama mtu fulani akimwekea mikono na kumfanya nabii. Nabii anazaliwa kutoka katika tumbo la uzazi la mama yake, ni nabii, unaona, kwa hiyo yeye daima ni nabii. Unaona?

194 Mungu alimwambia Yeremia, akasema, "Kabla hata hujachukuliwa mimba katika tumbo la mama yako," kasema, "nilikujua na kukutakasa na kukuweka nabii kwa mataifa." Hiyo ni kweli. Unaona? Musa, kabla hajazaliwa, yeye alikuwa ni mtoto mzuri. Yeye alikuwa ni nabii wa Bwana. Hao wengine wote wakitokea. Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, tangu bustani ya Edeni. Hiyo ni kweli. Unaona, karama na miito havina majuto.

195 Lakini karama zinatolewa kwa Mwili ule. Sasa tunatambua hilo, tunatambua karama hizi zote.

196 Sasa hebu tuone kile Yesu alichokuwa miongoni mwetu, tuone kile alichokuwa huko nyuma. Tunaona ya kwamba wakati alipoanza huduma Yake kwa mara ya kwanza . . . Sasa, sikiliza kwa makini, mgeni. Wakati alipoanza huduma Yake kwa mara ya kwanza, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, tuliona baada ya Yeye kubatizwa, baada ya Yeye kuja . . . Yeye alizaliwa na akafikia umri wa miaka thelathini, Yeye alibatizwa na Yohana. Roho Mtakatifu alishuka kama hua na akakaa juu Yake, ndipo Sauti ikaja na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa ambaye ndani Yake . . . " Kiyunani cha asili kilisema, "Ambaye ndani Yake ninapendezwa kukaa." Kasema, "Ambaye ninapendezwa, ambaye—ambaye ndani Yake ninapendezwa kukaa." Lakini, mnaona, hilo linasikika la kishamba kwetu, na kitenzi kabla ya kielezi, lakini kwa kweli ni, "Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake." Maana, Kristo, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa Nafsi Yake. Tunajua jambo hilo.

197 Sasa, mara alipoenda siku arobaini huko nyikani, akijaribiwa na ibilisi. Ndipo akatokea na huduma Yake, akaanza kuwaombea wagonjwa.

198 Baada ya kitambo kidogo, alitokea mtu jina lake Simoni Petro, mzee mvuvi, asiye na elimu, hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Andrea akamwambia kuhusu Jamaa huyu aliyeamini kwamba ni Masihi. "Upuuzi!"

199 Akamjia. Na mara alipoenda mbele za Yesu, Yesu alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Yeye alijua jambo fulani lilitukia. Alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Na ilimpendeza Yeye kumpa funguo za Ufalme, akamfanya kichwa cha kanisa.

200 Kulikuwako na jamaa mmoja aliyesimama pale, jina lake Filipo. Filipo aliona jambo hilo, naye akawazia, "Ajabu hii! Ninamjua mtu ambaye ni msomi wa Biblia, anaishi yapata maili kumi na tano nyuma ya mlima ule. Nitakimbia kule nikamwambie. Jina lake ni Nathanaeli."

201 Alikimbia kule upesi sana siku hiyo. Kesho yake asubuhi alifika kule, labda kwenye mapambazuko. Akakimbia na kubisha mlango. Ndipo Bibi Nathanaeli akasema, "Vema, yeye yuko huko nje kwenye bustani ya matunda huko nje, Filipo." Rafiki yake, akaenda huko nje, naye alikuwa amepiga magoti, akiomba. Mara aliposimama, Filipo akasema, "Njoo, umwone Mtu niliyempata! Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

202 Sasa huyu muungwana mashuhuri, wa kidini alisema, "Laweza neno jema kutoka Nazareti?" Yeye alimpa nukuu zuri, jambo zuri, alisema, "Usikae nyumbani na kulikosoa, usiende ukiongea juu yake. Njoo tu, ujionee mwenyewe. Njoo, uone! Njoo tu, ujionee kama neno jema linaweza kutoka Nazareti."

203 "Unataka kusema Masihi? Mbona, Masihi angekuja, angeshuka aje, na kushuka kutoka kwa ninii...Ushoroba wa Mbinguni ungeshushwa, Yeye angekuja moja kwa moja kwenye ikulu. Yeye angekuja kwa dhehebu letu kuu." Wangali wanawazia hilo, mnaona, halina budi kuja kwenye shirika lao. "Yeye angekuja moja kwa moja kwenye dhehebu letu, ashuke kwenye ushoroba wa ikulu pale. Naye angeenda kwenye nyua za nje na kuja moja kwa moja kwenye kiti cha enzi, na juu kwenye Patakatifu pa patakatifu, na kusema, 'Mimi Ndimi Masihi.'" Masihi kamwe haji namna hiyo. Masihi huja mahali anapotaka kuja. Yeye ni mkuu, Yeye hufanya apendavyo.

Akasema, "Vema," yeye akasema, "njoo uone! Njoo, ujionee mwenyewe."

204 Usisimame huku na kusema, "Siamini katika upuuzi huo wa watakatifu wanaojifingirisha." Njoo tu, ujionee kama kuna lolote kulihusu.

205 Kwa hiyo yeye, alipokuwa njiani akienda huko, ninaweza kuwasikia wakizungumza. Hebu, je! mngetaka kusikia yale waliyokuwa wakizungumzia? Hebu tutege masikio na tuone yale waliyosema. Ninaamini, wakienda zao wakipitia kando ya barabara, mwajua, Filipo alisema, "Unajua, Nathanaeli, ninajua wewe ni mwanafunzi wa Biblia, kwa hiyo ninataka kukuuliza jambo fulani. Tunamtazamia Masihi, sivyo?"

206 "Loo, naam, tunafikia kwenye siku za mwisho kwa ajili ya kizazi hiki na hiki, ninaamini ndicho kizazi kitakachomwona Masihi." Sasa sikilizeni. "Loo, lakini sisi hapa, sisi hata si taifa, sote tumetawanyika miongoni mwa watu. Tunawezaje? Haya yote!" Mungu huja kwenye saa usiyotarajia. Huo ndio wakati anapokuwapo.

207 Yeye alisema, “Lakini, ngoja kidogo, huyu Masihi atakuwa ni mtu wa aina gani?”

“Loo, Musa, mwalimu wetu, alitwambia Yeye atakuwa ni nabii.”

208 “Nitakwambia juu ya huyu Yesu wa Nazareti. Je! unamkumbuka maskini yule mzee mvuvi asiye na elimu uliyenunua wale samaki kutoka kwake wakati ule, ukaleta, ulinunua kutoka kwake, naye asingeweza kutia risiti sahihi, hakuwa na elimu ya kutosha?”

209 “Naam! Loo, loo, naam, a-ha. Yona na mvulana wa Yona. Naam, nilinunua kutoka kwa Yona, pia.”

210 “Vema, sasa, unajua nini? Petro alikuja kule. . . ” Ama Simoni, hasa, jina lake lilikuwa ni Simoni wakati huo. Yeye alisema, “Simoni alikuja kwenye mkutano Wake. Na mara alipoenda pale juu, yeye. . . Unakumbuka jinsi Simoni alivyokuwa akitwambia ya kwamba baba yake alimwambia ya kwamba ‘Asidanganyike, kwa kuwa kungekuwako na manabii wengi wa uongo kabla ya Masihi halisi.’ Na hiyo ni kweli. ‘Jumbe nyingi za uongo zitatokea.’ Lakini kasema, ‘Utajua wakati ule Ujumbe halisi utakapokuja, kwa sababu, kumbuka, sisi Wayahudi tunaamini ya kwamba Masihi huyu atakuwa ni nabii.’ Tunawaamini manabii wetu.”

211 Mwulize Myahudi sasa. Israeli, wanapoichukua hiyo Biblia pale pale sasa, wakitoka Irani na kadhalika, wanaisoma. Wanasema, “Kama huyo Yesu alikuwa ni Masihi, hebu tumwone akifanya ishara ya nabii, tutamwamini.” Naam, bwana. Wanajua hao manabii ni wa kweli.

212 Kwa hiyo hapana shaka Nathanaeli alisema, “Loo, ninaamini Masihi atakuwa ni nabii, maana Musa alisema, ‘Bwana Mungu wetu atatuondokeshea nabii.’”

213 “Vema, wakati alipoona jambo hilo, huyo Simoni ambaye unanena habari zake, Yeye alisema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Si kwamba tu Yeye alimjua, bali alimjua yule baba yake mzee Mfarisayo.”

“Aha! Siwezi kuamini hilo. Umepungukiwa na akili.”

214 Akasema, “Loo, la, sijapungukiwa! Hebu njoo, uone. Njoo, uone! Njoo huku!” Moja kwa moja barabarani, wakaenda.

215 Hatimaye akaenda kwenye Uwepo alipokuwa Yesu, labda amesimama kwenye wasikilizaji mahali fulani. Yesu akisimama pale, akiangalia kote. Baada ya kitambo kidogo akaangalia nje, Naye akamwona Nathanaeli amesimama pale nje, akasema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!” Hilo lilimshangaza sana. Hilo lilimtoa pumzi. “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

216 “Huyo ni Mungu,” akasema. “Rabi,” linamaanisha *mwalimu*, “Rabi, ulinijua lini? Sijakutana nawe hapo kabla, mimi ni

mgeni kwenye kusanyiko hili, sijapata kuwa hapa hapo kabla. Ungewezaje kunitambua?"

217 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona."

218 Huyo alikuwa ni Yesu jana. Je! hiyo ni kweli? Kama ni yeye yule, Yeye ni yeye yule leo. Hebu tulichukue taifa lingine la watu. Kulikuwako na taifa la watu . . .

219 Kulikuwako na mataifa matatu pekee ya watu, na hayo ni watu wa Hamu, Shemu na Yafethi. Unaona? Hiyo ni kweli kabisa. Hapo ndipo, kwenye Pentekoste, ambapo Injili iliwaendea Wayahudi, halafu kwa Wasamaria, na kisha kwa Wamataifa. Unaona, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, ndiyo—ndiyo hayo mataifa matatu. Sasa, kuna mataifa mawili ya hayo yanayomtazamia Masihi; sio sisi Wamataifa. Tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, tulikuwa makafiri, tukiziabudu sanamu; bali sio—sio Hamu na Shemu.

220 Sasa, kuna lingine sasa, ta—taifa hilo lingine lilikuwa ni Wasamaria, ambalo lilikuwa nusu Myahudi na nusu Mmataifa, lililosababishwa na dhambi ya Kora pale, nao wakaanguka. Nao walimwamini Mungu, walikuwa wakimtazamia Masihi. Kwa hiyo Yesu aliienda, akijionyesha mbele zao. Alikuja kwa Wayahudi, watu Wake Mwenyewe, bali alikuwa na haja ya kupitia Samaria. Yohana Mtakatifu 4, mlipata kuisoma? Naye alikuwa na haja ya kupitia Samaria. Kwa hiyo akafika kwenye mji wa Sikari, kwa hiyo akawatuma tu wanafunzi Wake kununua vyakula. Na wakati walipokuwa wameondoka . . .

221 Kama ulipata kuwa kule, ni mandhari nzuri sana, chemichemi, kuna kitu kama, pampu ya mji, mahali wanapoyachotea maji. Mwajua, wanawake wanakuja na kuchukua winchi na kuitelemsha ndoo chini, wanachota maji, wanayaweka kichwani mwao. Na sasa wanawake wenye sifa mbaya, wanawake wabaya, wasingekuja pamoja na wanawake wazuri. Hawakuwa na uhusiano siku hizo. Mwanamke aliyekuwa mbaya, alikaa kwenye kundi lake mwenyewe. Sivyo ilivyo leo; wote wako pamoja, bali wananinii tu . . . lakini wao, ni kama tu kudonoa katikati ya yai, unalifanya lote taa nyekundu, unaona. Kwa hiyo basi, wao, kwa hiyo wanajaza hii . . .

222 Mwanamke mwenye sifa mbaya alitokea huko nje, kama saa tano na nusu ama saa sita kasorobo, yapata wakati huu mchana, alikuja akitembea pale kuchota ndoo ya maji. Naye akaachilia . . . akaweka ninii . . . Ninaweza kumwona akiweka maskini ekseli hapa na winchi, akaitumbukiza kisimani, kuchota ndoo ya maji. Na yapata tu wakati alipoanza kuivuta juu, alimsikia mtu fulani akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Naye akaangalia hapo na huyo hapo Myahudi. Sasa, hawakuwa na uhusiano wowote mmoja kwa mwingine.

223 Mwanamume wa makamu, Yeye alikuwa na umri wa kama miaka thelathini. Lakini Biblia ilisema alionekana ni wa miaka hamsini, mnajua hilo. Alisema, "Unasema ya kwamba ulimwona Ibrahimu, na Wewe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini." Yeye alikuwa na umri wa miaka thelathini tu. Mnaona? Kasema . . . Nadhani huduma Yake ilimsumbua sana. Kwa hiyo akasema, "Unasema ya kwamba umemwona Ibrahimu, sasa tunajua ya kwamba Wewe una pepo."

224 Akasema, "Ibrahimu asijakuwapo, MIMI NIKO." Mnaona, Yeye ni Mungu wa Ibrahimu. Hakika, alikuwa. Akasema, "Ibrahimu asijakuwapo, MIMI NIKO." Hakika.

225 Na sasa, yule pale ameketi kisimani, akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

226 Akasema, "Si desturi. Tuna ubaguzi hapa." Kama waliokuwa nao huko Kusini, watu weusi na wazungu, mnaona. Yeye alisema, "Tuna ubaguzi hapa. Sio desturi Wewe kuniomba, Wewe (Myahudi) kuniomba (mwanamke Msamaria) kutoa fadhili yoyote, chochote kile. Hatuna ushirikiano sisi kwa sisi." Alikuwa ni maskini mwanamke kahaba, mwajua. Kwa hiyo, labda ni mwanamke mrembo. Naye alikuwa amesimama pale, labda nywele zake za kipilipili zimening'inia usoni mwake, mwajua, naye alikuwa nje usiku kucha. Na—na kwa hiyo alisema, naye akasema, "Si kawaida Kwako kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho."

227 Akasema, "Mwanamke, kama ulijua ni Nani alikuwa akisema nawe, na ulijua ni Nani ulikuwa ukisema naye, ungeniomba maji unywe." Huyo ni Masihi jana, unaona. "Ungeniomba maji unywe, ningekupa maji usije hapa kuchota."

228 "Mbona," akasema, "kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kuchotea, utanipaje maji yoyote?" Kasema, "Baba yetu Yakobo!" Unaona, yeye alikuwa ni Msamaria, bali alimwita Yakobo baba yake, pia. "Baba yetu, Yakobo alikinywea kisima hiki, ng'ombe wake, familia yake. Na hata hivyo unasema una maji mazuri kuliko haya?" Kasema, "Ninyi mnasema 'kuabudu,' Wewe ukiwa ni Myahudi, mnasema 'Yerusalemu.' Sisi tunasema katika mlima huu."

229 Akasema, "Mwanamke, wakati unakuja, na sasa upo, wakati ibada za kweli ataabudiwa Mungu katika Roho, maana Mungu ni Roho." Unaona? "Baba anawatafuta kama hao kufanya hivyo."

Yeye alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiongea naye, apate kuwasiliana na roho yake. Mnaona? Sasa, kumbukeni, Yeye hana budi kuwa ni Masihi, mbele zao Wasamaria. Na moja kwa moja akapata shida yake. Ni wangapi wanajua ilikuwa ni nini? Hakika. Yeye alikuwa akiishi na mume wake wa sita.

Kwa hiyo, unaona, ni makosa wakati una mume aliye hai, yuko ndani, na—na kadhalika, na kutoka. Na kwa kila sababu

tu, kumwacha mwanamke, na kumwoa, kisha kwenda kuoa mwingine, kuoa mwingine, kuoa mwingine, hupaswi kufanya hivyo. Kwa hiyo akasema, yeye . . .

Ndipo mwanamke huyo, nadhani alikuwa akiishi bila ya hata kuolewa nao. Huenda hakuolewa nao kamwe. Huenda kamwe hakupata kuolewa. Kwa hiyo alisema mambo haya yote maovu, mwajua, alifanya upuuzi huu wote mchafu.

Kwa hiyo basi wakati alipokuwa amesimama pale, akimwangalia namna *hiyo*, Yeye alisema, "Nenda, uniletee maji ninywe." Naye akasema . . . "Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema Naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Nitakuletea maji usije . . . Nitakupa maji, usije hapa kunywa." Ndipo akasema, "Nenda, ukamwite mume wako mje naye hapa."

Akasema, "Bwana, sina mume."

"Loo," Yeye akasema, "umesema vyema. Umekuwa na waume watano, na uliye naye sasa siye mume wako. Katika hilo umesema vyema." Yeye, sikilizeni, mwanamke huyo . . . Sasa wakati ninii . . .

Wayahudi walimwita nini wakati walipomwona akifanya hivyo? Je! walimtambua kuwa ni Masihi? La. Wao walisema yeye alikuwa ni nani? "Beelzebuli, mpiga ramli," kasema, "hizo nguvu zilikuwa Beelzebuli." Nao wakamwita Roho wa Mungu, aliyekuwa akifanya huo utambuzi, "kitu kichafu."

Akasema, "Ukisema neno dhidi Yangu, nitakusamehe. Lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja, kufanya jambo lile lile; nawe ukisema neno moja dhidi Yake, hutasamehewa hilo kamwe."

230 Kwa hiyo mnaona mahali tulipo leo hii; kama ikitokea kuwa ni leo hii. "Neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao." Kwa hiyo mnaona kile kizazi hiki kimefanya. Sasa wazia jambo hilo. Wazia kwa makini. Yapime Maneno haya yenye uchaji.

231 Sasa, Wayahudi walisema, "Mtu huyu anafanya mambo haya kwa Beelzebuli. Yeye ni ibilisi, mpiga ramli." Tunajua ya kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi. Kwa hiyo akasema, "Mtu huyu ni mpiga ramli."

232 Kwa hiyo aliwasamehe kwa kumwita mpiga ramli. Lakini baada ya Yeye kufa na Roho Mtakatifu kurudi, basi ilikuwa ni tofauti. Unaona? Na hiyo, hiyo ni kwa kizazi cha Mataifa. Sasa angalieni.

Sasa, Wa—Wayahudi tayari walikuwa wameliona, wakalihukumu.

233 Wasamaria walilipokea, naye akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni Nabii." Utafanya nini nalo, Msamaria? "Ninaona kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya." Mnaona, walimjua

Masihi, kwamba angekuwa ni Nani. Kasema, "Tunajua ya kwamba Masihi, ambaye anaitwa Kristo, atakapokuja Yeye atatwambia mambo haya. Lakini u Nani Wewe? Je! Wewe ni nabii Wake?"

Akasema, "Mimi Ndiye. Mimi Ndiye."

234 Basi aliposikia hili! Sasa sikilizeni. Aliposikia hili, aliacha mtungi wake wa maji akakimbia mjini, naye akaja kuwaambia watu mitaani, akikimbia kupitia mjini, kasema, "Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya! Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?" Nayo Biblia ilisema ya kwamba mji wote ulimwamini kwa sababu mwanamke huyu alikuwa amesema hivi, ya kwamba Yeye aliwaambia, maana Yeye alikuwa ni Masihi.

235 Sasa, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, Naye ni yeye yule, jana, leo, na hata milele, itakuwa ni ishara ile ile leo hii. Hiyo ni kweli? Ni wangapi watakaokubaliana na hilo? Hakika, ndiyo, ni ile ile. Vema.

236 Sasa, itakuwa ni mtu yeyote tofauti? La. Yeye alipenda, alilia, aliomboleza, alilala, alienda nyikani, alienda kuvua samaki, alifanya tu kama mtu mwingine yeyote. Alikuwa ni mwanadamu tu, unaona, bali hata hivyo alikuwa ni Masihi mtiwa mafuta.

237 Sasa, sasa tunakumbuka katika Biblia, inayotwambia huko nyuma, ambako tunayaendea Maandiko mengi na kuthibitisha ya kwamba Biblia inadai ya kwamba kutakuwako na "Siku ambayo haitakuwa ni usiku wala mchana," siku yenye utusitusi tu, madhehebu na kanisa, na ya kutosha kuokolewa, "bali wakati wa jioni itakuwa Nuru." Ni wangapi waliowahi kusoma hilo katika Biblia? Hakika. Mnaona?

238 Sasa, kwa maneno mengine, jua huchomoza Mashariki na kutua Magharibi. Jua lile lile linalochomoza Mashariki, hutua Magharibi. Vema, wakati Mwana wa Mungu, M-w-a-n-a, alipochomoza Mashariki, kwa watu wa Mashariki. Ustaarabu husafiri, husafiri pamoja na jua, nasi tuko katika Pwani ya Magharibi sasa. Kama ukivuka, unaenda Uchina, unarudi Mashariki tena. Kwa hiyo basi Mwana yule yule aliyeangaza Mashariki sasa anaangaza Magharibi, pamoja na ubatizo ule ule wa Roho Mtakatifu, ishara zile zile, maajabu yale yale, Masihi yule yule. Hiyo ni kweli? "Itakuwa Nuru wakati wa jioni, njia ya Utukufuni hakika mtaipata." Hiyo ni kweli.

239 Tuko jioni, Nuru ya jioni. Jua linatua. Masihi yuko miongoni mwetu. Mwana wa Mungu, katika umbo la Roho Mtakatifu, yuko katikati yetu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.] Mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? ["Amina."] Mnaamini ya kwamba yale ninayowaambia ni Kweli? ["Amina."] Mnaamini hadithi ya yule Malaika jana asubuhi, majuzi asubuhi? ["Amina."] Mnaiamini? ["Amina."] Basi hebu Mungu

wa Mbinguni, hebu Mungu aliyenitokea katika umbile la ule upinde wa mvua, hebu na anene. Na hebu na mwili wangu uwekwe wakfu Kwake, nafsi yangu, roho, na nia, ziwekwe wakfu kwa ajili ya utukufu Wake. Wakati nilipokuwa nikimtafuta yule kuchakulo wa mwisho, na nikijua angekuwa ndiye wa mwisho, wakati huo ilikuwa ni saa nne kasoro dakika tatu, nami nilikuwa nimesema ingekuwa ifikapo saa nne.

Mwajua, Yeye alisema, "Sema utakayo. Itakuwa hivyo." Yeye hajashindwa bado, chochote kile. "Sema tu utakalo."

Lakini mara ya nane hilo lilipowahi kufanywa, ilikuwa juu ya maskini mwanamke mmoja. Ameketi kule nyuma sasa, nadhani. Ninamwona Ndugu Wright ameketi hapa. Hattie Wright, wakati alipoomba kwa ajili ya watoto wake wawi-. . . Yule pale, pale pale sasa. Kwa ajili ya wokovu wa watoto wake wawili, (sivyo?) walipinga hilo kwa dhati. Nikasema, "Ninakupa watoto wako, katika Jina la Yesu Kristo." Wakaanguka moja kwa moja pajani mwake.

240 Ed Daulton, Mbaptisti anayeketi hapa, kutoka huko Kentucky, anayeketi papa hapa. Una watoto wangapi, Ed? Watoto kumi na wawili. Amesimama papa hapa, aliomba kwa ajili ya watoto wake. Nikatoka nje ya jengo. Ed akanijia tena; nikasema, "Ed."

Roho Mtakatifu alikuwa juu yangu, nikasema, "Mpe hao. Mpe."

241 Nikasema, "Ninakupa watoto wako." Kila mmoja wao, ameokoka na kubatizwa. Kulikuwako na tineja wake ameketi nyumbani, akingojea, akilia, ameokoka tangu alipokuwa hapa juu. Huyu ndugu Mbaptisti kutoka huko chini katika . . . Loo, loo, ni wa ajabu jinsi gani wakati Yeye anaponena!

242 Ninamwomba sasa, kwa ajili ya utukufu Wake, kujionyesha Mwenyewe, ya kwamba Yeye ni Kristo, ya kwamba ninasema Kweli.

243 Sasa, kusudi a—asiyeamini asipate njia ya kuepukia. Ninataka watu waliomo humu ndani, ambao ni wagonjwa na wahitaji, mnamhitaji Mungu, nisiowajua, wageni malangoni mwetu, watu nisiowajua, walio hapa, na wanamhitaji Mungu, inueni mikono yenu. Watu kila mahali. Hiyo, vema, karibu tu kila mahali, nadhani. Watu ambao siwajui. Kama nikimwita mtu anayejua, ambaye ninamjua nawe unanijua, na—na tunafahamiana, usiseme kitu, wewe tulia tu. Kama Yeye ni Mwana wa Mungu, ambaye Ndiye, na Ujumbe wangu ni wa kweli, na huyo Malaika . . .

244 Wakati ilipokuwa saa nne kasoro dakika tatu, nilisema, "Ee Mungu, ambaye alinitokea muda mfupi uliopita katika ule upinde wa mvua, ni dakika tatu. Sioni kuchakulo yeyote. Ni dakika tatu, itakubidi kuniletea mmoja." Naye Mungu akiwa ni Hakimu wangu, ninasema kwa uchaji huku mkono wangu

ukiwa juu ya Biblia. Siamini katika kuapa, Biblia haisemi hivyo; inasema tusifanye hivyo. Lakini Mungu ni Hakimu wangu, kuchakulo alishuka mbio moja kwa moja mtini na kuketi vizuri hasa. Yeye kamwe hajashindwa; kamwe hajapata kushindwa. Wengi wao hapa wapo kujua mambo hayo. Ninajua ya kwamba Yeye, Mungu yuyo huyo, yupo hapa.

245 Kuna kadi za maombi zilizosambazwa. Sizitaki. Tutawaacha waombewe katika dakika chache, watakuja katika mstari. Sitaki watu waliopo—waliopo hapa, ama wowote wale.

246 Ninataka wageni. Ninataka watu wasionijua mimi. Ninawatakeni mliweke niani mwenu, ninawatakeni mwende mkiwazia na kuomba, na kusema, "Mungu, mtu huyo hanijui mimi."

247 Na siku moja maskini mwanamke mmoja alipenyeza kwenye umati. Alikuwa anatokwa na damu. Naye akasema . . .

248 Wakati wote walipokuwa wakisema, "Huyu hapa! Hebu mwangalieni! Yule pale yule Mgalilaya," na kadhalika. Wote hao marabi na kadhalika wamesimama pale, wakisema, "Rabi, tunatafuta ishara kutoka Kwako," na kadhalika namna hiyo.

249 Maskini mwanamke huyu alisema, "Ninaamini Yeye ni Mwana wa Mungu. Nami ninaamini kama ninaweza tu kugusa pindo la vazi Lake, nitakuwa mzima." Ni wangapi wanaojua hilo? Yeye alimgusa.

250 Sio kwamba Yeye angehisi; bali alisimama na kugeuka, kasema, "Ni nani aliyenigusa? Mtu fulani alinigusa." Kila mtu akanyamaza kimya kabisa. Kasema, "Mtu fulani alinigusa." Kasema, "Ni nani aliyenigusa?"

251 Naye akaangalia kila mahali hata akampata maskini mwanamke huyo. Asingeweza kujificha. Asingempata. Akampata na kusema, "Imani yako imekuponya." Kasema, akamwambia, kutokwa kwake kwa damu kulikuwa kumeokolewa kwa saba-. . .imarishwa, kwa sababu alikuwa ameamini, na imani yake ililigusa vazi Lake. Mnaamini hilo? Vema.

252 Sasa, je! Yeye ni Kuhani Mkuu leo hii anayeketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, akituombea tunapokiri? Hivi Biblia inasema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Hiyo ni kweli? Vema, kama wewe ni mgonjwa, anza kuomba, useme, "Bwana Mungu, ndiyo kwanza niusikie Ujumbe. Si—simjui mtu huyu. Nipo—nipo hapa maskanini. Siji hapa, hili silo kanisa langu la nyumbani. Nimetoka mahali pengine. Nimetoka nje ya mji, nimetoka mahali pengine. Simjui mtu huyu. Lakini analifanya, anaonekana kulifanya dhahiri sana ya kwamba ni Wewe, naye amesema ya kwamba Wewe ulimtokea, ya kwamba Ujumbe wake ulikuwa ni wa kweli, na jinsi ambavyo Wewe unayafanya mambo haya. Sasa, simjui mtu huyu, bali ninakujua Wewe. Kwa

hiyo kama yeye amejiweka wakfu Kwako, na Wewe unautumia mwili wake kunena Maneno Yako Mwenyewe kumpitia, jalia aseme nami. Jalia niliguse vazi Lako, Bwana." Ndipo tuone kama Yeye atalifanya ama hatalifanya! Tuone kama Yeye ni Mungu.

253 Kama Yeye angali ni Mungu, Yeye anaweza kuitumia midomo yangu kusema maneno yale yale ambayo angesema, maana Yeye hana midomo ila yangu na yako. Hana macho ila yetu. Kwa hiyo Yeye hushuka tu na kuliendeleza Kanisa Lake kupitia kwa mwili wetu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kuliendeleza, Mwenyewe! Hivyo ndivyo Yeye alivyosema. "Kazi nizifanyazo Mimi, mtafanya zizo hizo." Hiyo ni kweli? ["Amina."] "Kazi zile zile, mtazifanya." Hizo zilikuwa ni kazi alizofanya, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Sasa, kama Yeye ni Masihi, Naye Ndiye, basi, hiyo ikiwa ni kweli, basi Yeye anafanya kazi zile zile sasa hivi, kupitia Kanisa Lake, alizofanya wakati huo. Hiyo inathibitisha kwamba ni kweli, bila kujali madhehebu yenu yote. Loo, haleluya!

254 Maskini mzee Ndugu Kidd na Dada Kidd wanaoketi hapa, wote wawili, nao wana umri wa miaka themanini, wakihubiri kabla sijazaliwa. Huyu hapa amelala hivi majuzi asubuhi, akifa, kwa kansa, yapata miaka miwili iliyopita, wakimfanyia upasuaji wa tezi dume; huko mbali Ohio. Wamekuwa ni marafiki wangu wasiri sana. Dada Kidd alinipigia simu, akasema, "Billy, afadhali uharakishe. Yeye yuafa tu, sasa hivi yuafa." Basi mimi na Billy karibu tulichome maskini lile gari langu la mtumba, tukielekea kule.

255 Nilipofika mle chumbani, mara nilipofika pale, Roho Mtakatifu akanena, "BWANA ASEMA HIVI."

256 Yule pale amesimama, shahidi wa utukufu wa Mungu, hata alimfanya daktari wake ashtuke sana. Ni ninii tu, Yeye ni Mungu! Ningeweza kufanya hivyo? La, bwana! Maneno yangu si zaidi ya ya mtu mwingine yeyote. Lakini hiyo ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI! Amina.

257 Miaka kadhaa iliyopita, huko chini kwenye milima ya Kentucky, maskini Church of God ndogo, ama baadhi yao, wakishuka na kupanda kwenye ubavu wa vilima, wakipiga mahindi kwa kipande cha fimbo, pamoja na maskini mzee mama Kidd, kulilisha kundi la watoto; akiosha kwenye beseni, apate kumpeleka mume wake hudumani.

258 Na hawa hapa katika umri wao wa miaka themanini na kitu, wameketi hapa juu leo hii, wakiifurahia Injili ya Yesu Kristo, wakiendesha gari maili mia moja na kitu Jumapili asubuhi, kila Jumapili ninayohubiri hapa chini, kama wanaweza kusikia habari zake. Hakika, huwatumia mialiko, wanataka kuja. Naitakia heri maskini mioyo yao mikongwe. Hiyo ni kweli. Ninamtaka kila mtu hapa ndani kuwapa mikono asubuhi ya leo, wakiweza, muwabariki.

Sasa ombeni.

259 Loo, nina furaha sana kujua ya kwamba Yeye ni Mungu. Ni hisi ya jinsi gani! Mnasema, "Kwa nini unasitasita, Ndugu Branham?" Ninamngojea. Ni. . .Nimekuwa nikihubiri. Huu ni upako mwingine.

260 Na kama Yeye atakuja na kufanya jambo hilo, ni wangapi humu ndani basi, walio wagonjwa, watamkubali kama mponyaji wao? Inueni tu mikono yenu, wagonjwa wote, kama Yeye ata— kama Yeye atalifanya. Inueni mikono yenu, kila mtu aliye mgonjwa, ambaye anaweza kuona ya kwamba huyo Masihi, Kristo, yuko miongoni mwa watu, akinena.

261 Ombeni. Aminini. Nitamakinia upande *huu* wa nyumba. Nina wengi sana wanaoomba. Ninauona ule upako.

262 Angalieni. Ni wangapi wameisikia ile, ile Nguzo ya Moto pale, ambayo sayansi imeitundika huko Washington, DC? Mnaifahamu. Hii hapa picha Yake, papa hapa, Nguzo ile ile ya Moto iliyomwongoza Musa. Wakati hata sayansi ilisema, "Siku moja itakuwa kwenye rafu za maduka ya mali-mali. Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha."

263 Malaika yeye yule yupo papa hapa mimbarani sasa hivi. Mtafuteni. Ninawapa changamoto kuamini. Ninyi watu wa nje, ninyi aminini.

264 Sasa inanibidi tu kuangalia mahali ninapoiona ikielekea. Iweni na kicho, kila mtu, katika Uwepo Wake, ule Uchaji.

265 Ninamwona mwanamume. Hii hapa. Ameketi mkono wangu wa kushoto, papa *hapa* nyuma pembeni. Yeye anaugua ugonjwa wa mapindi na ugonjwa wa tumbo. Wewe amini kwa moyo wako wote. Wewe ni mgeni kwangu. Huyo ni Bw. Wells. Hilo ndilo jina lako, Bw. Wells. Wewe hutoki hapa. Uko mahali panapoitwa Aurora, Illinois. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako. Simama kwa miguu yako. Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini sasa? "Kama unaweza kuamini."

266 Sasa, pale, huyo jamaa, sijapata kumwona maishani mwangu, na ni mgeni kabisa miongoni mwetu. Ametoka mkoa mwingine. Naye Roho Mtakatifu, sasa, lolote alilomwambia, sitajua mpaka nitakapoipata kanda hiyo. Ni upako unaokuja juu yako. Lakini mtu huyo anajua.

267 Yale uliyoambiwa ni kweli. Hiyo ni kweli, bwana? Naam. Hatufahamiani. Kuna, hebu yeye awe ndiye shahidi wa nafsi yake.

Ni nani aliyefanya hilo? Masihi, Kristo.

268 Huyu hapa mama anayeketi papa hapa nyuma hapa, katikati ya watu, papa *hapa*. Unaiona ile Nuru juu yake? Yeye anaugua ugonjwa wa ngozi. Bibi Pitman, umetoka Owensboro. Kama

wewe ni mgeni, punga mkono wako. Je! mambo hayo ni kweli? Punga mkono wako. Mungu alikuponya. Kamwe sijapata kumwona mwanamke huyo, bado, ila tu katika ono.

269 Kusudi mpate kujua, moja kwa moja kutoka kwako kuna mwanamke jina lake Ellis, Bibi Ellis, mwanamke kijana. Ana shida ya akina mama. Yeye ni mgeni pia. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako. Huyo ni mama yako anayeketi karibu nawe hapo? Ni mama anayeketi hapo, akiugua ugonjwa wa woga, hisia za woga juu yake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Vema. Woga huo umekwisha. Unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Ninakupa changamoto uamini.

270 Huko nyuma kabisa, pembeni, huko nyuma kabisa, mwanamume kutoka Minnesota, akiumwa na mgongo. Jina lako ni Bw. Carson. Simama kwa miguu yako. Ugonjwa wako wa mgongo umekwisha. Yesu Kristo anakuponya.

271 Papa hapa nyuma *hapa*, mama anaugua. Ametoka nje ya mji. Ametoka mahali panapoitwa Kisiwa cha Bluu. Ana Ugonjwa wa moyo. Huko ni karibu na Chikago. Bibi Braiden, simama, kubali uponyaji wako. Nenda nyumbani ukawe mzima, katika Jina la Yesu Kristo.

272 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vipi kuhusu sehemu *hii*? Mnajua huyo ni Masihi? Mtu atajuaje?

273 Watu hawa wote ambao wameitwa, umbali huu, na mnajua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, ninyi watu wote ambao mmeitwa, huku. Mnaona hapo?

274 Yupo mtu fulani nyuma yangu, anayeomba, nyuma, kwenye chumba. Ni jamaa mdogo, mwenye nywele nyeupe, akimwombea binamu huko Kansas, ana kansa. Njoo huku mbele mlangoni. Mwamini Mungu. Unaamini?

275 Elmer, huyo alikuwa na uhusiano na wewe. Ninamwona baba yako ameketi pale, mke wake. Shinikizo kuu la damu. Kama unaamini, Mungu atakuponya. Sijui. Hiyo ni kweli. Sivyo? Amini kwa moyo wako wote.

276 Unaamini? Unaamini ya kwamba Yesu Kristo ni Masihi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini Uwepo Wake upo hapa? ["Amina."] Kumbukeni, wakati mwanamke mmoja alipoligusa vazi la Yesu, Yeye alidhoofika. Nguvu, uwezo, ulimtoka. Mimi karibu nimekwisha sasa. Mnaamini? ["Amina."]

Basi hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi.

277 Ee Yesu, Masihi wa Mungu, Wewe daima uko karibu. Watu wanafahamu ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, ya kwamba Wewe upo hapa sasa. Ishara Zako kuu na maajabu yanathibitishwa. Wabariki, Baba. Wabariki, ninaomba. Wajalie sasa hivi kuamini, kwa moyo wao wote, kwamba Wewe, Masihi, Ndiye unayesimama hapa. Hakuna mtu angaliweza kufanya jambo hilo. Hilo haliwezekani kibinadamu, Bwana.

Mwujiza, kuziona nguvu za Masihi zikiingia mahali padogo, panyenyekevu kama hapa, kwa sababu Wewe uliliahidi, Bwana. Kwa sababu, neema Yako iko hapa kutufunika. Kwa sababu ni ahadi Yako kufanya hivyo, Wewe umelifanya. Tunaona ya kwamba Wewe huwaachi watu Wako.

278 Sasa, Baba, Mungu, jalia wale walio na kadi za maombi, wakiingia kwenye mstari wa maombi, jalia wawe na imani kuamini. Ee Mungu Mwenyezi, wakati wanapowekelewa mikono, jalia waingie hapa ndani, wakifurahi, wakishangilia, wakimsifu Mungu, ya kwamba wameponywa. Tujalie, Bwana.

279 Na jalia hawa ambao wameokolewa, wajue ya kwamba hakuna siri kwa Mungu. Mungu huzifunua siri za moyo; Yeye anajua kila wazo lililo moyoni mwetu. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

280 Sasa, ninyi mlio na kadi za maombi, huko kwenye wasikilizaji, ninyi watu mnaoizunguka maskani, kote kupitia *hapa*, mlio na kadi za maombi, je! mnaamini? Inueni mikono yenu. Na mwamini ya kwamba mwanadamu hawezi kufanya hayo. Hayo hayana budi kutoka kwa Mungu. Mnaamini ni ahadi ya Mungu, ya kwamba Mungu alisema angelifanya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Basi mnajua ya kwamba mtu Fulani yupo hapa mbali na mwanadamu.

281 Kwa uchaji ninalichukua Neno hili, mbele za Mungu. Watu walionenewa, wowote wale, siwajui mimi, wala hawanijui. Hao ni wageni ambao walikuja tu maskanini hapa, popote walipokuwa.

282 Nimeona maono juu ya watu hapa walio kwenye maskani, bali nikawaacha, naam, nikawaacha tu.

283 Hao watu walioitwa, wowote wale, ili kwamba wengine wapate kuona ya kwamba ninyi ni wageni, inua mkono wako. Mnaona? Kila mmoja, wote wageni.

284 Kitu fulani kinaendelea tu kunisukuma. Ninamwona mama mweusi akitokea mbele yangu, wakati wote, ana yabisi kavu na shinikizo kuu la damu. Naam. Wewe ni mgeni miongoni mwetu. Umetoka Memphis, Bibi Sals. Hilo ndilo jina lako. Hii ndiyo mara yako ya kwanza hapa. Unamwamini Bwana, kwa moyo wako wote? Basi unaweza kwenda nyumbani na uokolewe, uponywe. Mungu anamshughulikia.

285 Amini kwa moyo wako wote, kila mtu. Inueni mikono yenu sasa, kila mtu. Aminini kwa mioyo yenu yote. Wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine.

Njoo hapa, Ndugu Neville. Njoo hapa, omba dua.

286 Wakati tukiinamisha vichwa vyetu, Ndugu Neville ataomba.

Ujumbe Wa Neema SWA61-0827
(The Message Of Grace)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 27 Agosti, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org